# Nipashe

Jumamosi Mei 13, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581309

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,112,462,859

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Askari wa TANAPA wanaodaiwa kupiga wananchi kikaangoni

UKURASA 3




UKURASA 11

# NYOTA IMEZIMIKA



BERNARD K. MEMBE 1953 – 2023

## ... Samia, Mwinyi, Mbowe wamlilia

### • **Familia**, daktari, msaidizi wafunguka *Endelea Ukurasa 2*



"Kwa zaidi ya miaka 40, ndugu Membe alikuwa mtumishi mahiri wa umma, mwanadiplomasia, mbunge na waziri aliyetumikia nchi yetu kwa weledi."- **Rais Samia Suluhu Hassan.**



"Sifa zake za uongozi na utumishi wa umma zitakumbukwa daima." – **Dk. Hussein Ali Mwinyi.**



"Mheshimiwa Membe aliitumikia nchi yetu katika ngazi mbalimbali na alikuwa hazina muhimu kwa taifa." – **Freeman Mbowe.**



."Alikuwa mtu wa maamuzi... Membe wakati wa uhai wake aliipenda Tanzania." **Kapteni George Mkuchuika.**



"Alikuwa na tabia ya kusimamia, kutetea kile alichokiamini. Akiliamini jambo alikuwa analitetea na alikuwa tayari kufa nalo." – **Nape Nnauye.**

**MICHEZO** YANGA YAJIPANGA KUFUNGA HESABU UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waombolezaji wakimfariji Doricas Membe (kushoto) ambaye ni Mjane wa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe, nyumbani kwake, Mikocheni B, Dar es Salaam, jana. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# Nyota imezimika ghafla

**Na Romana Mallya**

NYOTA imezimika. Maneno haya yanaashiria kuwa mwanasiasa, mwanadiplomasia nguli na aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, hatunaye tena.

Membe alifariki jana katika Hospitali ya Hurbert Kairuki, Mikocheni, Dar es Salaam, alipokuwa akipatiwa matibabu baada ya kuzidiwa ghafla.

**DAKTARI AFUNGUKA**

Daktari Bingwa na Mshauri Mwandamizi wa Magonjwa ya Ndani na Magonjwa ya Moyo kutoka Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), ambaye ni daktari wa familia ya Membe, Prof. Harun Nyagori, aliwatoa hofu Watanzania kuwa kifo chake ni cha kawaida.

Akizungumza na waandishi wa habari, Prof. Nyagori alisema kifo chake kimetokana na maambukizi ya mfumo wa mapafu hewa, ugonjwa ambao unasababisha mgando wa damu na kuzuia mapafu kupeleka hewa ya oksijeni.

"Kwa kifupi labda nieleze sababu kubwa zilizofanya Membe kufariki dunia. Mheshimiwa Membe alikuwa mzima na alikuwa na afya inayoimarika miaka yote. Hajawahi kuwa na tatizo lolote sugu labda presha. Magonjwa yoyote ya moyo, sukari, hajawahi kuwa nayo," alisema.

Alisema Membe alipata maambukizi ya ghafla ya mfumo wa mapafu ambayo yalisababisha kutengeneza mgando wa damu kuwa nzito na kuzuia mapafu kupeleka oksijeni.

"Niondoe tafrani au niondoe mchanganyiko ambao umekuwa ukizungumzwa huko mtaani kwamba Mheshimiwa Membe ameuawa, amepewa sumu. Hiyo imani iondoke hiki ni kifo cha kawaida ambacho mwanadamu yeyote kingeweza kumkuta hata mimi mwenyewe," alisema.

Daktari huyo alisema Membe alianza kupata tatizo hilo juzi kama homa ya kawaida, kifua na akawa anapata dawa zake kama kawaida lakini ghafla usiku wa kuamkia jana, alipata shida ya kupumua ikaonekana apelekwe hospitalini.

**MSAIDIZI ANENA**

Msaidizi wa Membe, Jerome Luanda, alisema alikuwa na bosi wake huyo juzi mpaka saa 6:00 usiku na kwamba pamoja na kupata dawa, alikuwa katika hali ambayo haikuonyesha kwamba angekumbwa na umauti.

"Saa 10:00 alfajiri mama (mke wa Membe) alinipigia simu kuwa mzee amezidiwa, anakohoa mfululizo na kukosa pumzi, hivyo nije haraka. Nilipofika tulimpeleka hospitalini na hatimaye akaaga dunia," alisema.

**KUZIKWA JUMANNE**

Msemaji wa familia, Jaji Mustafa Ismail, akizungumza jana nyumbani kwa marehemu, Mikocheni, alisema maziko yake yanatarajiwa kufanyika Jumanne ijayo saa 9:00 alasiri kijijini kwao Rondo, Mtama mkoani Lindi.

Alisema kesho kutakuwa na utoaji wa heshima za mwisho zitakazofanyika katika Viwanja vya Karimjee, jijini Dar es Salaam kuanzia asubuhi hadi saa 9:00 alasiri.

**HISTORIA YAKE**

Membe ambaye alizaliwa Novemba 9, 1953 Rondo, mkoani Lindi, akiwa ni mtoto wa pili kati ya watoto saba waliozaliwa katika familia ya Mzee Kamillius Anthony Ntachile na Mama Cecilia John Membe, alianza elimu ya msingi mwaka 1962 katika Shule ya Msingi Rondo-Chiponda na kuhitimu mwaka 1968.

Baada ya hapo alijiunga na masomo ya sekondari katika seminari ya Namupa (1969-1972), baadaye kuendelea Itaga Seminari, Tabora kwa masomo ya kidato cha tano na sita mwaka 1973 hadi 1974.

Mwaka 1975 aliajiriwa serikalini hadi 1980 Ofisi ya Rais na mwaka 1981 hadi 1984 alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa masomo ya Shahada ya Kwanza katika Sayansi ya Siasa na Uhusiano wa Kimataifa.

Baada ya kuhitimu, alirejea kazini na kufanya kazi hadi mwaka 1989 na mwaka uliofuata alijiunga na masomo ya shahada ya uzamili katika Uchumi, Uhusiano ya Kimataifa na Sheria za Kimataifa Chuo Kikuu cha John Hopkins, Marekani.

Alipohitimu mwaka 1993 alirudi serikalini kuendelea na kazi kama mchambuzi wa mambo ya ulinzi na usalama na baadaye kufanya kazi za kidiplomasia katika balozi mbalimbali.

**SIASA**

Membe aliingia katika siasa mwaka 2000 kwa kugombea ubunge katika jimbo la Mtama na kukaa katika wadhifa huo kwa miaka 15 mfululizo.

Mwaka 2015 aliacha kugombea ubunge na kujitosa katika kinyang'anyiro cha urais na kuwa katika nafasi tano za wanachama wa CCM waliofikishwa katika mchujo ndani ya Halmashauri Kuu ya Taifa. Yeye na January Makamba walienguliwa na kubaki Dk. John Magufuli aliyeshinda nafasi hiyo, Dk. Asha Rose Migiro na Balozi Amina Salum Ali.

Katika serikali ya awamu ya nne chini ya Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, alishika nyadhifa za Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, na Nishati na Madini kabla ya kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa miaka minane hadi mwaka 2015. Alikuwa mtu wa pili kwa kushika wadhifa huo kwa miaka mingi, akitanguliwa na Kikwete aliyeshika kwa miaka 10.


KUPOTELEWA NA CHETI



**GERALD MSILANGA MATINDI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S156/009** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **TANGA TECHNICAL SEKONDARI** mwaka 1984. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **IR/IRI/RB/125325/2023.**



JANHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA

SHAURI LA MADAI NA. 9/2022

PETER PHILIP SIMWIMBA (Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Judith Jordan Simwimba).....MDAI

DHIDI YA

REGINO LUHERO CHAULA........................MDAIWA WA KWANZA

TUGU COMPANY LIMITED.................................MDAIWA WA PILI

NATIONAONAL INSURANCE CORPORATION OF TANZANIA.....................................................MDAIWA WA TATU

ATTONEY GENERAL.......................................MDAIWA WA NNE

Kwa : REGINO LUHERO CHAULA.

POPOTE ULIPO -TANZANIA.

Unatarifiwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Tarehe 24/05/2023 siku ya Jumatano Saa3:00 Asubuhi bila ambapo Shauri limepangwa kusikilizwa.
ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila wewe kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 04 Mwezi MEI,Mwaka 2023.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MBEYA


## ... Samia, Mwinyi Mbowe wamlilia

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI na wanasiasa mbalimbali, wakiwamo Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wamemlilia Waziri wa zamani wa mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe wakisema alama aliyoiweka katika utumishi haitafutika.

Membe alifariki dunia jana asubuhi katika Hospitali ya Hurbert Kairuki, Mikocheni, Dar es Salaam baada ya kuugua ghafla.

Kutokana na kifo hicho, Rais Samia katika ukurasa wake wa Instagram jana aliandika kuwa: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha ndugu Bernard Membe.

"Kwa zaidi ya miaka 40, Ndugu Membe alikuwa mtumishi mahiri wa umma, mwanadiplomasia, mbunge na waziri aliyetumikia nchi yetu kwa weledi. Pole kwa familia, ndugu, jamaa na marafiki. Mungu amweke mahali pema. Amina."

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, katika salamu zake za rambirambi, alisema amehuzunishwa na taarifa za kifo cha Membe ambaye alikuwa kiongozi mwenye uwezo mkubwa, mwanadiplomasia hodari na mtumishi shupavu wa taifa.

"Marehemu aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Sifa zake za uongozi na utumishi wa umma zitakumbukwa daima," alisema.

Kutokana na msiba huo, Dk. Mwinyi alitoa pole kwa familia, marafiki na wote walioguswa na msiba huo.

**MBOWE ASIKITIKA**

Katika ukurasa wake wa Twitter, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Nje, Mheshimiwa Bernard Membe.

"Mheshimiwa Membe aliitumikia nchi yetu katika ngazi mbalimbali na alikuwa hazina muhimu kwa Taifa. Raha ya milele umpe ee Bwana na mwanga wa milele umwangazie. Apumzike kwa amani."

**NAPE NA MKUCHIKA**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu, Kazi Maalum, Kapteni Mstaafu George Mkuchika, alisema Membe alikuwa ndugu yake na kwamba katika maisha yake alifanya kazi mbalimbali ndani ya serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) ikiwamo Mkuu wa Idara ya Mambo ya Nje ndani ya chama.

"Mimi natoka Mtwara yeye Lindi, hivyo tulikuwa tunashirikiana. Ninavyomfahamu alikuwa ni mtu wa maamuzi, wakati wote alipenda kupumzika kijijini kwao na kuzungumza na wanakijiji," alisema Mkuchika.

Alisema Membe wakati wa uhai wake alipenda Tanzania, alifanya kazi katika balozi mbalimbali, alikuwa hodari na mchapakazi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema: "Mara ya mwisho kuzungumza naye hazijapita siku nne, kwetu sisi wanamtama ni msiba mkubwa."

Alisema Membe alikuwa kaka yake kwa sababu alimlea kisiasa tangu akiwa mdogo na ndiye aliyemfunza siasa.

"Kwetu sisi msiba huu ni mkubwa sana, alikuwa ni mpezi wa maendeleo kwa watu wa kusini na taifa. Alikuwa na tabia ya kusimamia, kutetea kile alichokiamini kwamba akiamini jambo alikuwa analitetea na alikuwa tayari kufa nalo," na kuongeza kuwa suala la jambo analoliamini ndilo ambalo amewaachia vijana.

Mbunge wa Isimani (CCM), William Lukuvi, alisema amefanya kazi na Membe kwa muda mrefu ndani ya CCM na serikali na kwamba alikuwa rafiki yake na mwanafamilia.

"Nimekuwa naye bungeni, baraza la mawaziri, tumekua pamoja katika siasa ndani ya CCM. Ni mtu aliyebarikiwa na Mungu kujua mambo mengi, ukimfuata na ajenda yoyote alikuwa anaijua," alisema.

Lukuvi alisema Membe alikuwa ni mtu mwepesi kumfikia wakati wowote, kwamba taifa limempoteza mtu aliyekuwa mshauri.



Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akiwasilisha makadirio ya bajeti ya wizara hiyo, kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024, Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Askari TANAPA wanaodaiwa kuwapiga wananchi kikaangoni

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, amemwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo, kuwachukulia hatua za kinidhamu maofisa wote wa serikali walioshiriki kwenye tukio la udhalilishaji wananchi wa kijiji cha Mwanadhali, Mbarali mkoani Mbeya.

Hatua hiyo inakuja ikiwa ni siku moja baada ya agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alilolitoa bungeni jijini Dodoma, kutokana na Mbunge wa Mbarali (CCM), Francis Mtega, kudai kwamba wananchi hao wamefanyiwa vitendo vya ukatili na maofisa wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA). Mbunge huyo alidai kuwa wananchi hao walidhalilishwa na kupigwa na askari hao baada ya mifugo yao kuingia hifadhini.

Katika madai hayo, mbunge huyo alisema wanawake wa kijiji hicho walivuliwa nguo na kubaki watupu kisha kuunguzwa mwilini na panga lenye moto, huku vijana wakipigwa na wafugaji kuporwa zaidi ya mifugo 250.

Katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Mchengerwa akiwa katika kikao na wananchi hao jana, alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbasi, kuwachukulia hatua za kinidhamu maofisa wote wa serikali walioshiriki kwenye migogoro hiyo.

Waziri huyo amewaomba wananchi kuzingatia sheria na kuwataka kutovamia maeneo ya makazi ambapo katika mgogoro huo, baadhi yao walikutwa kilomita kumi ndani ya Hifadhi ndipo walipoanza kutolewa kwa nguvu na wahifadhi.

Katika kikao hicho, Mchengerwa alitoa mkono wa pole wa Sh. milioni moja kwa wananchi watano kila mmoja kama kifuta machozi kutokana na ugomvi wa wahifadhi na wananchi hao.

Aidha, alisema tatizo la mipaka katika hifadhi hiyo linakwenda kumalizika na kwamba, Jumatatu anatarajia kutia saini GN mpya ya mpaka wa eneo hilo.

Waziri Mchengerwa alisema mipaka ya hifadhi hiyo iliwekwa mwaka 1910 wakati ikijulikana kama Saba Game Reserve na mwaka 1946 ikijulikana kama Hifadhi ya Rungwe na mwaka 1964 kama Hifadhi ya Ruaha ikiendelea hadi sasa.

"Dhamira ya serikali ni kuona kuwa kero zote katika maeneo ya hifadhi zinatatuliwa kwa amani na upendo.

"Ibara ya 68 ya CCM inasisitiza uhifadhi wa rasilimali, hivyo sisi sote tunapaswa kushirikiana kwa pamoja tuhifadhi kwa faida ya kizazi cha sasa na baadaye," alisema.

Katika kikao hicho, Ngalao Laini aliiomba serikali kuangalia namna bora ya kuwahamisha wananchi na kuwatengea maeneo bora ya makazi pindi inapoamuliwa kuwaondoa katika hifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya ambaye pia aliambatana katika ziara hiyo na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, na Wilaya ya Mabarali na viongozi wa CCM wa wilaya hiyo, aliwaambia wananchi kuwa serikali itahakikisha watu wote wanatendewa haki ikiwa ni pamoja na kufanya tathimini za makazi na kuwalipa fidia stahiki.

Katika maagizo yake juzi, Majaliwa alisema: "Ninaiagiza Wizara ya Maliasili na Utalii sasa hivi popote walipo, Waziri, Katibu Mkuu na Mtendaji Mkuu wa TANAPA waende mkoani Mbeya kukutana na Mkuu wa Mkoa.

"Kwa kuwa tulipokuwa Mbarali na kutoa maelekezo ya vijiji vyote vilivyokuwa na mgogoro wa GN 28 kulikuwa na vijiji zaidi ya 32. Baada ya Mapitio kuona yale maeneo kama je yana tija kwa wakulima au kwa hifadhi tuliridhika kwamba vijiji 27 havina tija."

# Mikakati 13 kuboresha huduma za afya

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WIZARA ya Afya inatarajia kutekeleza mikakati 13 kuboresha huduma za afya, ikiwamo kudhibiti magonjwa hatari ya kuambukiza na ya mlipuko huku Sh. bilioni 20.7 zikitengwa kutekeleza jukumu hilo.

Waziri mwenye dhamana, Ummy Mwalimu, aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24 huku akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.2 katika kutekeleza mikakati hiyo.

Ummy alisema katika mwaka huo wa fedha, wizara yake itaimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa zikiwamo huduma za chanjo, lishe, usafi, afya, mazingira na huduma za afya ngazi ya jamii.

"Tutaimarisha utekelezaji wa afua za chanjo kwa watoto nchini ikiwamo kununua, kutunza na kusambaza chanjo, kununua majokofu 1,601 ya mnyororo baridi wa chanjo, kununua magari 102 ya kusambazia chanjo, kuimarisha huduma za lishe," alisema.

Kadhalika, alisema wataimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa na vituo vya umma katika ngazi zote.

Pia alisema wataimarisha upatikanaji na udhibiti wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi na damu salama katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya na kwamba Sh. bilioni 205 zimetengwa.

Alisema wataimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na vya watoto wachanga.

Waziri alisema wataimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi ili kusogeza huduma hizo karibu na wananchi na kuwapunguzia gharama za kupata matibabu hayo nje ya nchi.

Kadhalika, alisema wataimarisha huduma za afya ya akili, huduma za utengamao na tiba shufaa, kudhibiti magonjwa ya mlipuko na magonjwa hatari ya kuambukiza. Pia alisema watadhibiti magonjwa ya kuambukiza hususani malaria, kifua kikuu, VVU/UKIMWI na homa ya ini.

Mkakati mwingine, alisema ni kudhibiti magonjwa yasiyo ya kuambukiza na kuimarisha huduma za dharura nchini ikiwamo ajali, kuimarisha upatikanaji wa wataalam katika sekta ya afya katika fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi.

Alisema wizara itaendeleza na kusimamia huduma za tiba asili na tiba mbadala nchini, wataimarisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na matumizi ya takwimu.

Sambamba na hilo, alisema wizara itaimarisha Ummy mifumo ya ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kusimamia utafiti na matumizi ya matokeo ya utafiti mbalimbali katika masuala ya afya.

# Magonjwa mfumo wa hewa bado tishio

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu amesema katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, mwaka huu, magonjwa ya maambukizi katika mfumo wa hewa ni miongoni mwa magonjwa 10 ambayo yaliongoza katika kuwaathiri zaidi wananchi.

Amesema magonjwa hayo ndiyo yamewafanya wananchi wengi kwenda katika vituo vya huduma kupata matibabu katika kipindi hicho. Waziri Ummy aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka 2023/24, akiliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 1.2.

Magonjwa ya maambukizi katika mfumo wa hewa, alisema yameathiri wananchi kwa asilimia 24 yakifuatiwa na magonjwa ya njia ya mkojo kwa asilimia 13 na malaria kwa asilimia saba.

Alisema kwa mwaka 2021/22 magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ya maambukizi ya mfumo wa hewa kwa asilimia 23, yakifuatiwa ya njia ya mkojo asilimia 13 na malaria asilimia nane.

Ummy alisema magonjwa yaliyoongoza watu kulazwa na asilimia kwenye mabano ni malaria (11), homa ya mapafu (10, anaemia (6.2) ikilinganishwa na na kipindi kama hicho mwaka 2021/22 ambapo homa ya mapafu ilikuwa asilimia 11.6, malaria (11.5) na anaemia (6.4).

Ummy alisema katika kipindi hicho magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa nje (OPD) wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa kwa asilimia 37.3, malaria (10.69) na kuharisha pasipo kupungukiwa maji mwilini (8.39). Alisema kwa umri wa miaka mitano na zaidi magonjwa yalikuwa ni maambukizi katika mfumo wa hewa kwa asilimia 18.8, maambukizi katika njia ya mkojo (16.1) na malaria (6.5).

"Magonjwa yasiyoambukiza yanaongezeka kwa kasi hadi kufikia kuwamo katika orodha ya magonjwa 10 yanayoongoza kusababisha watu kuhudhuria katika vituo vya kutolea huduma za afya." Alisema Ummy.

Ummy alisema katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, magonjwa yaliyoongoza kwa wagonjwa wa kulazwa (IPD) kwa wenye umri chini ya miaka mitano yalikuwa ni homa ya mapafu kwa asilimia 25.5, malaria (19.18) na kuharisha (13.8). Alisema kwa upande wa wagonjwa walio na umri wa miaka mitano na zaidi, magonjwa yaliyoongoza yalikuwa ni malaria kwa asilimia 13.8, maambukizi katika njia ya mkojo (9.77) na shinikizo la juu la damu (8.92). Kuhusu utoaji wa huduma za matibabu, Ummy alisema serikali imeendelea kusimamia utoaji wa huduma za matibabu kwa wananchi, katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi, 2023, wagonjwa 35,873,466 walipatiwa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Alisema wagonjwa 34,298,339 walikuwa ni wa nje na wagonjwa 1,575,127 walilazwa.

# Kizimbani madai utakatishaji bil. 1.4/-

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa Nepal, Cameroon na Watanzania watatu wamepandishwa kizimbani na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi yenye mashitaka saba, likiwamo la utakatishaji wa Sh. bilioni 1.4.

Washitakiwa hao ni Bhusal Govinda, na Emanuel Gaudios, raia wa Nepal, Takoounga Anselme, raia wa Cameroon na Watanzania Raymond Richard, Caroline Magafu na Grace Sureshi, walifikishwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Akisoma hati ya mashitaka, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grolia Mwenda, akisaidiana na Wakili wa TAKUKURU, Thuwaiba Hussein, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio wa mahakama hiyo, alidai kuwa watu hao wanashtakiwa kwa mashtaka saba.

Mwenda alidai kuwa Agosti na Septemba, 2022 ndani ya jiji la Dar es Salaam, washitakiwa kwa pamoja na kwa nia ovu, walijiunga na mtandao wa kihalifu na kujipatia Dola za Marekani 623,000 sawa na Sh. 1,449, 098,000 kutoka kampuni ya Zhejiang Afol Import and Export Co. Ltd.

Alidai kuwa kati ya Agosti 19 na Septemba 29, 2022 jijini Dar es Salaam, Magafu na Bhusal walijipatia Sh. bilioni 1,449, 098,000 kutoka kampuni hiyo kupitia akaunti yao iliyoko benki ya Stanbic kama malipo ya kuuza madini aina ya shaba tani 100, kupitia kampuni ya Steca Export and Import, wakati wakijua si kweli. Ilidaiwa kuwa kati ya Agosti na Septemba, 2022 ndani ya Dar es Salaam, Gaudios, Richard na Sureshi walikula njama ya kutenda kosa la kughushi.

Mwenda alidai kuwa Septemba 16, 2022 mtaa wa Nkrumah, mshitakiwa Gaudios alighushi hati ya kusafirishia mzigo (bill of lading), akionyesha kwamba,kampuni ya Stecas Export and Import imesafirisha tani 44 za shaba kwenda kampuni ya Zhejiang Afol Import and Export Co.Ltd wakati akijua si kweli.

Pia alidai katika tarehe hizo na eneo hilo, mshitakiwa huyo alighushi hati ya kusafirishia mzigo, akionyesha Stecas Export and Import imesafirisha tani 66 za shaba zimesafirishwa kwenda kampuni ya Zhejiang Afol Import and Export Co.Ltd wakati akijuasi kweli.

Ilidaiwa kuwa Septemba 2, 2022 eneo hilo, mshitakiwa huyo akiwa mwajiriwa wa kampuni ya Glob Vest Group Ltd, alijipatia fedha kutoka Zhejiang Afol Import and Export Co. Ltd kama malipo ya kusafirisha mzigo tani wa 44 za madini ya shaba.

Katika shitaka la utakatishaji fedha, ilidaiwa kwamba, kati ya Agosti 19 na Septemba 29, 2022 jijini Dar es Salaam, washtakiwa wote walijihusisha katika miamala ya Sh. 1,449, 098,000 wakati wakijua fedha hizo ni mazalia ya makosa ya jinai.

Baada ya kusomewa mashitaka hayo, Hakimu Mrio aliwaeleza washitakiwa hao kuwa hawaruhusiwi kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Wakili Mwenda alidai upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kutajwa.

Hakimu huyo aliahirisha kesi hiyo hadi hadi Mei 25, mwaka huu, kwa kutajwa na kuamuru washtakiwa wote wapelekwa mahabusu kwa sababu shtaka la utakatishaji fedha halina dhamana.



Mwanafunzi akisoma daftari la masomo yake, huku mkono mmoja akiwa ameshika bomba ndani ya daladala la Tegeta Nyuki – Gerezani, wakati akielekea shuleni katika Barabara ya Bagamoyo, Dar es Salaam jana. **PICHA: EMMANUEL KWITEMA**

# Baba adaiwa kuua mwanawe kwa fimbo

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

JESHI la Polisi mkoani hapa linamshikilia John Musoma (30), mkazi wa Kijiji cha Nkonko wilayani Manyoni, kwa tuhuma za kumuua mtoto wake, James Musoma (6) na kumjeruhi mwingine kwa kumpiga fimbo kichwani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutabihirwa, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 4, mwaka huu, kwa madai ya kumuua mtoto huyo na kumjeruhi mwingine Joseph Musoma (8).

Alisema sababu za mtuhumiwa huyo kuwapiga watoto wake hao ni baada ya kuchelewa kufika shambani kufukuza ndege wanaoshambulia zao la iweke.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutahibirwa, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani baada ya uchunguzi wa tukio hilo kukamilika.

Kamanda Mutabihirwa alitoa wito kwa wazazi na walezi kuacha vitendo vya ukatili vinavyoambatana na vipigo kwa watoto wao, kwani vinaweza kugharimu maisha ya watoto.

# Waajiri wasiotoa mikataba wakabwa koo

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, imeanza kufanya ukaguzi na kuwachukulia hatua waajiri wanaokwepa kuwapa mikataba wafanyakazi kwa kuwatumia kama vibarua ili kunyonya haki zao.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Patrobas Katambi, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza ya Mbunge wa Viti maalum (Chadema), Sophia Mwakagenda.

Mbunge huyo alisema kuna viwanda kwenye Mkoa wa Pwani maeneo ya Mbagala na Mkuranga wanawapa wafanyakazi Sh.4,000 kwa siku.

"Mfanyakazi anaingia saa mbili asubuhi hadi saa 11 jioni anapata ujira wa Sh.4,000 hii ni sawa? Serikali mnasimamia vipi matajiri na waajiri wakubwa ambao wanadaiwa na wafanyakazi madeni ya muda mrefu, kama kampuni ya chai ya Rungwe, mgodi wa Kiwira, TANESCO (Shirika la Umeme Tanzania) waliokuwa vibarua takribani sasa ni miaka mitano hawajapata fedha zao?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Katambi alisema serikali imebaini wako waajiri wanakwepa kuwapa mikataba ya kazi wafanyakazi ili kuendelea kuwaita vibarua na kuendelea kufanya kazi kwa muda mrefu ni unyonyaji mkubwa.

"Ofisi ya Waziri Mkuu imeanza kuchukua hatua na tunafanya ukaguzi kujua historia ya wafanyakazi wamefanya kazi kwa kipindi gani na aina ya kazi anayoifanya ili kuwaingiza kwenye mifumo ya kuwa na mikataba ya kazi ili haki zao zilindwe kwa mujibu wa sheria," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema katika sheria ya ajira na mahusiano kazini inaeleza moja ya mambo ni kukubaliana yawe kimkataba na yaandikwe na kuwekwa wazi.

"Kitendo cha waajiri kutolipa mishahara au masilahi yao ni kuvunja sheria ya ajira na mahusiano kazini, na ndani ya mkataba kuna masuala ya kodi ya mapato, asipolipa inamaana anakwepa kodi ya serikali na kuna kipengele cha lazima kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, asipolipa mshahara anakwepa pia kupeleka fedha kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii.

"Kuna kipengele cha Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) kwa hiyo asipolipa mishahara anamkosesha haki mfanyakazi ya kulipwa na tumekuwa tukiwapeleka mahakamani," alisema,

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji lini serikali itahakikisha Watanzania wanaofanya kazi kwenye kampuni za Kichina wanalipwa vizuri kwa mujibu wa sheria.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa sheria za kazi ili kulinda haki za wafanyakazi.

Pia alisema katika kuendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa sekta binafsi, Serikali kupitia Bodi ya Kima cha Chini cha Mshahara katika Sekta Binafsi imefanya utafiti na kuboresha kima cha chini cha mshahara kwa sekta binafsi.

"Viwango hivyo vipya vya Mishahara vilitangazwa kupitia Gazeti la Serikali Namba 687 la tarehe 25 Novemba, 2022 na utekelezaji wake umeanza rasmi tarehe 1 Januari, 2023," alisema.

Alisisitiza serikali kwa kushirikiana na taasisi nyingine zinazohusika na masuala ya kazi itaendelea kuhakikisha kuwa waajiri wanatekeleza ipasavyo viwango vya mishahara vilivyotangazwa kwa kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maeneo ya kazi na kutoa elimu kwa waajiri na wafanyakazi ili kujenga uelewa wao katika kutekeleza Sheria za kazi.

"Ofisi imeendelea kuchukua hatua dhidi ya waajiri wanaobainika kukiuka Sheria za Kazi hususan ulipaji wa mishahara kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kwa mujibu wa Sheria," alisema.

## Wauguzi waonywa lugha chafu dhidi ya wagonjwa

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WAUGUZI katika Manispaa ya Shinyanga, wametakiwa kuwahudumia wagonjwa kwa upendo pamoja na kutumia lugha nzuri za staha badala ya kuwatolea lugha chafu.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga, Dk. Elisha Robert, alisema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani, ambayo wauguzi wa Manispaa ya Shinyanga walifanyia kwenye Kituo cha Afya Kambarage. Maadhimisho hayo yalienda sambamba na kupanda miti na kutoa zawadi za sabuni kwa kinamama waliojifungua. Alisema wauguzi wa Manispaa ya Shinyanga katika kumuenzi muuguzi wa kwanza duniani, Florence Nigtngale, ambaye alikuwa akihudumia wagonjwa wa upendo, ni vyema wakamuenzi kwa vitendo kutoa huduma bora pamoja na kutumia lugha nzuri ambazo pia zinaongeza faraja kwa wagonjwa. "Natoa wito kwa wauguzi wa Manispaa ya Shinyanga mfanye kazi kwa kumtanguliza Mungu na kupokea vizuri wagonjwa. Tumieni lugha nzuri, mfanye kazi kwa bidii, ushirikiano, na kupunguza vifo vikiwamo vya uzazi," alisema Dk. Robert.

Katibu wa Afya Manispaa ya Shinyanga, Dk. Emmanuel Kabelwa, aliwataka wauguzi wafanye kazi kwa weledi, bidii na kwa ushirikiano ili kuokoa afya za wananchi.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**NGOMENI ENTERPRISES, AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKERS LIMITED na JADA INVESTMENT LIMITED,** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | KITWANA TWALIB JONGO | KITWANA TWALIB JONGO | NYUMBA YENYE HATI YA MAKAZI/ HATI | PLOT NO 49 BLOCK 10,MABWEPANDE ,MANISPAA YA KINONDONI | 22/05/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | JADA INVESTMENT LIMITED |
| 2 | AHMED HUSSEIN ABDULKARIM | AHMED HUSSEIN ABDULKARIM | NYUMBA YENYE HATI YA MAKAZI/ HATI | PLOT NO 135 BLOCK G,CHANIKA,MANISPAA YA ILALA | 25/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NGOMENI ENTERPRISES |
| 3 | LEONARD J BALYAGANGE | BWANA NA BIBI LEONARD J BALYAGANGE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA GOLANI KATAYA KIMARA,MANISPAA YA UBUNGO | 26/05/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NGOMENI ENTERPRISES |
| 4 | JOEL M GUMBO | JUDITH JOHNSON GUMBO | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NA.ILA009722 | NYUMBA YENYE LESENI NA ILA009722, ARDHI NA ILA/KWN/YMB15/104A, KIWALANI YOMBO,MANISPAA YA ILALA. | 27/05/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | NGOMENI ENTERPRISES |
| 5 | SALUMU R. MSUYA | AMINA M. SALEHE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO S/MTAA | MTAA WA MSAKUZI KUSINI KATA YA MBEZI WILAYA YA KINONDONI | 31/05/2023, SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKERS LIMITED |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

| NGOMENI ENTERPRISES | AMA'Z AUCTION MART & GENERAL BROKES LIMITED | JADA INVESTMENT LIMITED |
|---|---|---|
| P. O. Box 36359 | P. O. Box 62163 Dar es Salaam | P. O. Box 69098 |
| Dar es Salaam | Tel:0658100737, 0757276263 | Dar es Salaam |
| Tel: 0753575752/ 0784252048 | Email:amazauctionma@gmail.com | Tel: 0788493699, 0774501313 |
| | | Email:jadainvestmentlimited@gmail.com |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usajili wa wachezaji wapya Bara uzingatie na malengo

**WAKATI** pazia la Ligi Kuu Tanzania Bara likielekea ukingoni, kila timu imebakisha michezo mitatu ili kufunga pazia la msimu wa 2022/2023.

Mbali na ligi hiyo ya juu kwa upande wa Tanzania Bara, Ligi Kuu ya Zanzibar pia imebakiza michezo minne wakati Ligi ya Championship pia nayo inaelekea mwishoni, timu zinazoshiriki zimebakiza mechi mbili ili kumaliza hesabu.

First League au Ligi Daraja la Pili kama inavyojulikana sasa, tayari imeshamalizika na Cosmopolitan kutwaa ubingwa.

Kumalizika au kuelekea ukingoni kwa msimu huu, ni dalili sahihi ya kuruhusu taa za kuanza maandalizi ya msimu mpya zinatakiwa kuwashwa kwa timu zote ambazo zinahitaji kufanya vizuri katika msimu mpya.

Timu inayoanza mapema maandalizi yake kuanzia kusajili wachezaji na kupanga programu za kambi na kuiandalia timu yake mechi za kirafiki, basi hujiweka katika nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya kwenye msimu mpya.

Viongozi kusubiri kufanya mchakato wa usajili katika dakika za lala salama, ni dalili mbaya na ni nadra sana timu husika kupata matokeo chanya. Katika kuhakikisha suala muhimu la usajili linafanyika kwa mafanikio, huu ni wakati kwa viongozi wa klabu kuwapa uhuru makocha kukamilisha zoezi hili kwa kuangalia mapungufu ya kiufundi na si kufanya tofauti.

Mchakato wa usajili ukifanyika chini ya usimamizi wa makocha, utakwenda kwa weledi na utaisaidia timu husika kufanya vizuri na kufikia malengo katika mashindano mbalimbali ambayo itashiriki na vile vile itawasaidia walimu wa timu za taifa kupata wachezaji sahihi ambao wataipa matunda mazuri nchi.

Umefika wakati kila klabu ikawa na malengo ya kutwaa ubingwa kwa kusajili wachezaji wenye viwango vya juu na kuacha kuendelea kuwa wasindikizaji katika Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League, Ligi Kuu Zanzibar, Kombe la Azam Sports Federation, Kombe la ZFF na michuano mingine mbalimbali wanayoshiriki.

Kusajili wachezaji wazuri ambao wataipa timu malengo, si tu kutaitangaza klabu husika, lakini pia kutazifanya ligi zote kuwa na ushindani na kuzivutia kampuni na taasisi kudhamini, na kwa kufikia hatua hiyo, zawadi nono zitatolewa kwa washindi huku maofisa wanaosimamia pia kulipwa stahiki zao kwa wakati.

Tunapenda kuzikumbusha klabu kuacha tabia ya kusajili wachezaji dakika za lala salama, tunaamini kila timu tayari kwa asilimia zaidi ya 80 sasa imeshafahamu mapungufu yake, hivyo zinatakiwa kuanza mchakato wa usajili mapema lakini kwa kuzingatia na kuheshimu sheria na kanuni zilizowekwa.


Wakati klabu zikionyesha ubabe kutoa ofa kubwa kwa wachezaji wa kigeni, viongozi mnatakiwa pia kuwapa malipo yanayostahili nyota wazawa ambao wameonyesha mchango mkubwa kwa timu husika na kutoruhusu malumbano kama ya kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto' na klabu yake ya Yanga yatokee, huu ni wakati wa kukaa na wachezaji kwa ajili ya kufanya tathmini ya kazi waliyoifanya huku pia isiwaonee huruma wake ambao wanashindwa kujituma na kupata namba katika timu.

Kama ambavyo wachezaji wageni huja Tanzania kufanya majaribio na timu za hapa ili kuwashawishi kusajiliwa, huu pia ni wakati kwa nyota wetu pia kujitangaza nje kwa kusafiri au kutuma picha zao za video kupitia mawakala ambao wanafahamika rasmi na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA).

Klabu zifahamu kama wao huacha wachezaji kwa sababu ya kutofikia malengo, vile vile wawe tayari kuwaruhusu nyota wao kuondoka na kwenda kutafuta changamoto mahali kwingine bila ya kuwapo na migongano na hii itasaidia kila upande kufikia malengo yake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kufungia baa, kumbi ni kifo cha muziki wa dansi

**HIVI** majuzi Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC ), lilizifungia zaidi ya kumbi na baa 89 kwa kile kilichodaiwa kukiuka sheria za uchafuzi wa mazingira, hasa ikiwa ni kupiga muziki kwa sauti za juu.

Sitaki kwenda huko kwa undani kwa sababu nao wanafuata sheria, lakini jambo hili limeathiri vitu mbalimbali ikiwamo biashara za watu wengine pamoja na uchumi.

Hilo limebainishwa pia naTaasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) ambako nalo lilitoa taarifa ikisema kitendo cha NEMC kufunga biashara za baadhi ya baa na kumbi za starehe jambo ambalo limeathiri biashara nchini.

Likabainisha kufungwa kwa baa hizo 89 kumeathari mnyororo mzima wa biashara ikiwamo wasanii, wanamuziki, viwanda vya vinywaji, chakula, wavuvi, wasafirishaji na wakulima hivyo kupoteza zaidi ya ajira 5,000 pamoja na upotevu mkubwa wa mapato (kodi) kutokana na biashara hizo kufungwa.

Binafsi nasema kila mtu anafahamu athari ya uchafuzi wa mazingira hasa wa kelele na madhara yake, na inaheshimu mifumo iliyopo inayolinda mazingira, ila utekelezaji wa sheria na kanuni unafaa kufanyika kwa weledi, haki na usawa kwa wote.

Kufungia tu baa kumewafanya watu wengi kukosa ajira kwa siku hiyo na tunafahamu wateja wanapopatikana ndipo wanapolipwa.

Mimi nitajikita zaidi kwa wanamuziki wa dansi, ambao wanategemea zaidi baa na kumbi ili kujipatia kipato na riziki zao za siku.

Muziki ni kazi kama kazi nyingine yoyote ile ambayo inawafanya watu kuishi na kutunza familia. Muziki hauwezi kupigwa sehemu nyingine yoyote zaidi ya baa au kwenye kumbi za burudani.

Tunapozifunga, au kuziambia baa ziwe na kipimo kidogo sana cha sauti, hapo moja kwa moja ni kuua muziki wa dansi, huwezi kupiga muziki wa 'laivu' kwa sauti ndogo kama mtu mwenye redio ya mkulima 277.

Halafu wenye mabaa wanadai kuelezwa kutengeneza 'sound proof', kwa kweli hii inatumia gharama kubwa sana na wenye kumbi za starehe hawawezi kuingia gharama hizo, eti tu kwa sababu ya kuzifanya bendi zije kupiga.

Hapa moja kwa moja ni kama kuzipiga marufuku bendi za muziki wa dansi na wanamuziki wasifanye kazi, labda mpaka wakati wa kampeni za vyama vya siasa.

Kitendo hicho cha NEMC tayari kimeigusa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Chama cha Muziki wa Dansi (CHAMUDATA), na vingine vyote vinavyosimamia masuala la burudani.

Muziki wa dansi Tanzania una heshima kubwa tangu zama za Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ambapo ulitumika katika kudai uhuru, ukombozi Kusini mwa Afrika, kumng'oa Nduli Idd Amin, kuhamasisha mambo mbalimbali ya kizalendo, hivyo ulipaswa kuenziwa kama wenzetu wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo wanavyofanya.

Wakongo hata iweje, wanauheshimu muziki wao wa dansi na wanamuziki pia. Mara baada ya tukio hili, wiki nzima wanamuziki wamekuwa hawana kazi yoyote na kuanza kulalamika mitaani kwani wamiliki wa kumbi na baa wamewagomea katakata bendi zao kupiga kwa hofu ya kukamatwa na kufungiwa biashara zao.

Nadhani imefika wakati NEMC kukaa na wadau mbalimbali hata Wizara husika, ikiwamo hata wanamuziki na wasanii kuona watafanyaje kwa hili.

Kusema baa zipige muziki wa sauti ndogo, moja kwa moja umewaua wanamuziki na wasanii pia.

Meza na mazungumzo hayajawahi kushindwa, NEMC wanatakiwa kukaa na kuangalia pande zote mbili zisiathirike.

Wanaweza kukubaliana bendi zipige kuanzia saa 12 hadi saa sita usiku, baada ya hapo basi, lakini kusema zisipige kabisa ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Je wanamuziki wakapige wapi? Halafu hata baadhi ya kumbi wanazopiga zinazodaiwa kulalamikiwa na wakazi, zilikuwa mbali nao, ila wenyewe ndiyo wamezifuata.

Huko nyuma wakati muziki wa dansi uko juu, kumbi nyingi zilikuwa nje kidogo ya mji, lakini kwa sasa zipo katikati ya majumba ya watu, halafu wao ndiyo wanalalamika kelele. Watu ndiyo wamezifuata kumbi.

## HABARI KITAIFA

# EWURA yahamasisha uvunaji maji ya mvua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imewataka madiwani wa Jiji la Dodoma kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa uvunaji wa maji ya mvua kutokana na hali ya upatikanaji wa maji kwenye jiji hilo kutoridhisha.

Mkurugenzi wa Maji na Usafi wa Mazingira wa EWURA, Mhandisi Exaud Fatael, alisema hayo jana alipokuwa akifungua mkutano wa madiwani hao kuhusu umuhimu wa matumizi ya vyanzo mbadala vya maji jijini hapa.

Alisema pamoja na hatua ambazo EWURA imeendelea kuchukua, hali ya upatikanaji wa maji jijini Dodoma imekuwa si ya kuridhisha na kwamba Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA) kwa sasa ina vyanzo vya maji vyenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 67.1 kwa siku wakati mahitaji ya maji kwa siku ni lita milioni 133.844.

"Hii inapelekea (inasababisha) upungufu wa lita milioni 66.744 ya mahitaji ya maji kwa siku. Hata hivyo, asilimia 28 ya maji yanayozalishwa hupotea. Kutokana na upungufu huo na maji yanayopotea, huduma ya maji inapatikana kwa wastani wa saa 10 tu kwa siku," alisema.

Fatael alisema vyanzo vya maji katika Jiji la Dodoma ni visima virefu ambavyo uzalishaji wake hautoshelezi mahitaji hivyo maji hutolewa kwa mgao kwa wastani wa saa 12 kwa siku.

"Hivyo jitihada kubwa zinahitajika kukabiliana na upungufu huu wa maji ili kukidhi mahitaji ya huduma ya maji kwa wakazi wa Dodoma ikiwemo kuhamasisha matumizi ya vyanzo mbadala vya maji kama uvunaji wa maji ya mvua,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema utekelezaji wa suala hilo unahitaji ushiriki wa wadau mbalimbali kama Mamlaka za Serikali za Mtaa katika kutafuta suluhu ya kuimarisha hali ya huduma ya maji. "Aidha, madiwani wanayo nafasi ya kutunga sheria ndogo ndogo, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wake na kutoa elimu, inatoa rai kwenu, madiwani, kutoa hamasa kwa wananchi mnaowasimamia katika maeneo yenu, kuweka mikakati ya kuvuna na kuhifadhi maji ya mvua, wakati hatua mbalimbali za kuimarisha huduma ya maji zikiendelea kuchukuliwa na DUWASA,"alisema.

Naye Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe, alisema jiji litahakikisha linatumia elimu hiyo ya EWURA ili wananchi kuona thamani ya kila tone la maji na kuyavuna.

# Mbunge apigia debe posho wenyeviti vijiji na vitongoji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeombwa kuangalia uwezekano wa kutoa posho kwa wenyeviti wa mitaa, vijiji na vitongoji kutokana na baadhi yao kuanza kujitafutia kipato kwa kuuza viwanja na kusababisha migogoro kwa wananchi.

Ombi hilo lilitolewa bungeni jana na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mwandabila.

Akiuliza swali bungeni, Mbunge huyo alisema posho hiyo itasaidia watekeleze majukumu yao kikamilifu.

"Naomba serikali iwafikirie viongozi hawa kwa kuwa wengine kutokana na kutokuwa na posho wamejitafutia njia nyingine za kujipatia kipato ikiwemo kuuza viwanja na kusababisha migogoro kwa wananchi,"alisema.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na viongozi hao katika kutoa huduma kwa wananchi.

Ndejembi alisema kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura ya 290, kila halmashauri inatakiwa kuweka utaratibu wa kuwalipa posho, wenyeviti wa vijiji, mitaa na vitongoji kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani ya halmashauri.

Alisema serikali inaendelea kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili ziweze kubuni na kuimarisha vyanzo vya mapato pamoja na kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha kwa kutumia mifumo ya kieletroniki ya kukusanya na kutumia fedha katika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na matumizi mengineyo.

"Kwa mujibu wa sheria posho hizi zinatakiwa zilipwe kutoka kwenye mapato ya ndani ya Halmashauri," alisema.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alisema wenyeviti hao ndio wanaosimamia miradi ya serikali katika maeneo yao hivyo kama serikali haoni haja ya kuwalipa posho ya usimamizi.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alieleza kuwa amepokea ushauri huo na kwamba serikali itaangalia endapo bajeti itaruhusu.




Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Daikin, Toshiharu Surumaru (kushoto) na Mkurugenzi wa vituo vya Don Bosco Tanzania, Fr Fredrichk Swai wakizindua rasmi kituo cha ufanisi cha Chuo cha Ufundi cha Don Bosco, Dar es Salaam juzi, kinachofadhiliwa na kampuni ya Daikin ili kuwapa wanafunzi maarifa zaidi katika teknolojia mpya ya viyoyozi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Nsekela ataka uwazi vyama vya ushirika

**Na Joseph Mwendapole**

MWENYEKITI wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini (TCDC), Abdulmajid Nsekela, amewataka viongozi wa vyama vya ushirika nchini kufanyakazi kwa uwazi na weledi ili kuvifanya vyama hivyo kuwa endelevu.

Amesema binafsi kwa nafasi yake atasimamia ushirika kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha hautetereki na kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi.

Aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza kwenye kongamano lililoandaliwa na Jukwaa la Ushirika Mkoa wa Dar es Salaam, lililokuwa na kaulimbiu ya 'Ushirika kwa Maendeleo Endelevu.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wakuu wa vyama vya ushirika wa wilaya za Kinondoni, Kigamboni, Temeke, Ilala na Ubungo zote za mkoa wa Dar es Salaam.

"Huwezi kuwa na maisha endelevu bila kujali misingi ya kanuni na sheria ya uendeshaji wa maisha yako, kwenye ushirika uaminifu na uwazi ni mambo makubwa ya kuzingatia kama mnataka kufanikiwa," alisisitiza Nsekela.

Alisema vyama vya ushirika vimefanya mambo makubwa nchini katika kuikomboa nchi kijamii, kisiasa na kiuchumi, hivyo wanaosimamia vyama hivyo wanapaswa kutanguliza uzalendo.

Tanzania, aslisema haina uhaba wa wataalamu wa ushirika kwa kuwa serikali ilianzisha Chuo cha Ushirika Moshi mkoani Kilimanjaro ambacho kimekuwa kikizalisha wataalamu wengi mwaka hadi mwaka.

Alisema ingawa baadhi ya vyama vya ushirika vinakabiliwa na changamoto mbalimbali za uendeshaji, kuna vyama vya ushirika ambavyo vimekuwa vikisifika kwa kufanya vizuri ikiwemo Ngome na Tanesco na kuvitaka vyama vingine kuiga mfano huo.

Nsekela alisema serikali kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imejipanga kuendelea kusimamia kwa nguvu zote vyama vya ushirika nchini ili viendelee kutoa mchango kwenye uchumi.

"Mimi ni muumini wa mabadiliko, lakini mabadiliko hayaanzi na ushirika bali yanaanza na wewe mwenyewe, wote mlioko hapa ni viongozi lakini lazima mtambue kuwa taswira ya mabadiliko inaanza na mtu mmoja mmoja," alisema. "Mara ya kwanza nilipokutana na mrajisi wa vyama vya ushirika nilimwambia wazi kwamba waliotupa heshima hii ya kushika hizi nafasi wanataka kuona mabadiliko kwasababu ushirikia ni chombo kinachoweza kuleta maendeleo ya nchi na maendeleo ya mtu mmoja mmoja," aliongeza.

Alisema serikali inadhamira ya dhati ya kuboresha na kuendeleza ushirika nchini nan ndiyo sababu imekuwa ikitumia vyama vya ushirika kama nyenzo muhimu ya kusuma maendeleo hapa nchini.

Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Dk. Benson Ndiege, alisema vyama vya ushirika bado vinachangamoto kubwa hasa kwenye kufanya mambo yake kwa uwazi.

Alisema ushirika ni imani kwa hiyo watu wanapoona mambo yanaendeshwa kibabaishaji wanaweza kupoteza imani kwa vyama hivyo na kuamua kujitoa.

Dk. Ndiege alisema mpaka sasa vyama vya ushirika ambavyo vimeomba leseni nchi nzima vinafikia 1,185 na kati ya hivyo, vyama 789 ndivyo vimekidhi vigezo vya kupata leseni kwa mujibu wa sheria ya vyama hivyo.

Pia alisema vyama 386 vimeelekezwa kuboresha taarifa zao ili viweze kukidhi vigezo vya kupata leseni.

Alisema kwa mkoa wa Dar es Salaam, takwimu zinaonyesha kuwa kati ya vyama 500 vya akiba na mikipo ni 200 pekee vilivyoomba na kupata leseni.



Meneja Mauzo wa kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Paul Msuku (kushoto), akikabidhi nyaraka za mtambo wa kuchimbia madini na barabara aina ya XCMG kwa Mkurugenzi wa kampuni ya ujenzi ya Asa-General Supplies Ltd, Said Mnyagura, baada ya kuununua kupitia punguzo maalumu lililotolewa na GF kwa wateja wake wakati wa maonyesho ya madini jijini Mwanza juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bandari kuongeza uwezo kupokea shehena

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), inatarajia kujenga magati matatu likiwamo la kupokea makontena (makasha) na kuifanya kuwa na uwezo wa kuyapokea kufikia milioni 2.5.

Pia inatarajia kujenga gati maalum ya kuhudumia watalii na ya kuegesha meli za abiria.

Hayo yalisemwa juzi Dar es Salaam katika mkutano wa siku tatu, uliolenga kupitia mradi huo ulioko kwenye hatua ya upembuzi yakinifu na usanifu.

Mkutano huo ambao ulifungwa jana ulikutanisha wadau mbalimbali wa bandari, TPA yenyewe na wataalam washauri waelekezi kutoka kampuni ya Khatib & Alami (KA), ambayo ndiyo mshauri wa mradi huo.

Wataalam hao waliwapitisha hatua kwa hatua ya utekelezaji wa mradi huo na wadau wa sekta mbalimbali walikutoa ushauri wao na kupokelewa kwa ajili ya hatua nyingine.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Kaimu Mkurugenzi wa Mipango ya Miundombinu na Uwekezaji wa TPA, Ntandu Mathayo, ambaye ni Meneja Mradi huo, alisema kwa sasa mamlaka inafanya maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam kwa kuiboresha miundombinu iliyopo na kuongeza mingine.

"Maboresho yanayofanyika sasa yanatakayofanywa yanaifanya bandari kuwa na uwezo wa kuhudumia mzigo hadi kufikia tani milioni 28. Baada ya miaka 10 ijayo uwezo huo utafikiwa. Ili kujiandaa na mzigo unaokuja siku zijazo ndio maana tunataka kujenga gati la kupokea meli za makasha.

"Kwa sasa maboresho yanayofanyika bandari itakuwa na uwezo wa kubeba makasha 1, 150,000 baada ya miaka 10 ijayo tunatarajia mzigo utaongezeka. Ukiangalia miaka 12 iliyopita 2012 mpaka 2022 shehena la makasha limeongezeka kwa asilimia 110," alisema.

Alisema mwaka 2012 mzigo uliobebwa wa makasha kupitia bandari ya Dar es Salaam ulikuwa makasha yasiyozidi 450,000 na mwaka 2022 yalikuwa zaidi ya 880,000.

Mathayo alisema gati linalotarajia kujengwa hivi karibuni kutokana na upembuzi yakinifu unaofanywa na wataalam hao, litaongeza uwezo wa bandari wa kubeba makasha 1,350,000.

"Kwa maana hiyo ukichukua uwezo wa sasa wa bandari na baada ya kujengwa kwa gati hili, tutakuwa na uwezo wa kuhudumia kontena milioni 2.5.

"Teknolojia itakayotumika kwa sasa vifaa tunavyotumia kuhudumia mizigo bandarini vinatumia mafuta ya dizeli. Kwa kuzingatia hali ya mazingira duniani ambayo ndio ajenda kubwa ya mabadiliko ya tabia nchi, tunatarajia vifaa vyote vinavyohudumia makasha vitatumia teknolojia mpya ya umeme," alisema.

Kuhusu gati ya kuhudumia meli za watalii alisema kwa sasa bandari haina miundombinu hiyo na kutokana na nia ya serikali kuufanya mji wa Dar es Salaam kuwa wa kitalii, TPA imeamua kuijenga ili kuhudumia maeneo yote yanayozunguka jiji hilo zikiwamo mbuga za wanyama na visiwa vya Zanzibar na Pemba.

Alisema ujenzi wa gati utategemea na ushauri watakaopokea kutoka kwa mtaalam huyo mwelekezi anayefanya upembuzi yakinifu.

Meneja Mradi kutoka KA, Chadi Sabra, alisema wao ndio wanaosimamia ujenzi wa magati 12 mpaka 15 ya kusimamia meli.

"Tumefanya mkutano huu ambao umeisha leo ukihusisha mazungumzo na TPA kwamba ni vitu gani vinahitajika na tumewapa ripoti. Ila tumekutana na wadau hawa kote nchini kuwaambia vitu gani vinahitajika," alisema.

Hata hivyo, alisema wanafanya kazi kwa karibu na TPA kuhakikisha bandari ya Dar es Salaam inaongeza mzigo na kuliweka jiji hilo kuwa kituo cha utoaji huduma hiyo kwa ubora ndani na kwa nchi inazoizunguka.

Meneja wa kampuni hiyo upande wa Tanzania, Gloria Mushi, aliishukuru TPA kwa kuwaamini na kwamba wamekutana na wadau tofauti wakiwamo Wizara ya Utalii, Shirika la Reli Tanzania (TRC), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mwakilishi wa Katibu Mtendaji wa Shoroba ya Kati, Faraja Kondo alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuamua kufanya maboresho ya bandari na kuwataka wadau waendelee kuitumia Bandari ya Dar es Salaam.

# Wazalishaji wakumbushwa ubora bidhaa

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZALISHAJI nchini wametakiwa kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa viwandani, zinazingatia kanuni bora za uzalishaji ambazo hazitachafua wala kuharibu sifa halisi za bidhaa husika.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela, kwenye hafla ya utoaji leseni na vyeti 113 vya ubora kwa wazalishaji ambao bidhaa zao zimethibitishwa kukidhi matakwa ya viwango kwa kipindi cha kuanzia Aprili, 2022 hadi Machi, 2023.

Leseni na vyeti hivyo vilitolewa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kwa wazalishaji hao wa Kanda ya Kaskazini inayojumuisha mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga na Manyara.

Mongela kwa niaba ya wakuu wa mikoa hiyo, alisema ili kutekeleza hilo serikali imeendelea kutoa elimu kwa wadau wa kisekta kwa lengo la kulinda afya za watumiaji na mazingira katika Mkoa wa Arusha, Kanda ya Kaskazini na maeneo mengine nchini.

"Kupitia utekelezaji wa shughuli za TBS kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya mwaka 2009 pamoja na marekebisho yake kupitia Sheria ya Fedha Na. 8 ya mwaka 2019, tunashuhudia namna serikali inavyohakikisha ustawi wa wananchi wake kwa kulipia gharama za uthibitisho wa ubora na usalama wa bidhaa za wajasiriamali wadogo," alisema.

Kwa kipindi cha Aprili, 2022 hadi Machi, 2023, alisema Sh. 182,500,000 zimetumika kuwahudumia wajasiriamali wadogo 54 wa Kanda ya Kaskazini. Alisema lengo la hatua hii ni kukuza viwanda na uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla na kulinda afya za wananchi na mazingira.

Mongela aliipongeza TBS kwa kazi kubwa inayofanya katika uthibiti na udhibiti wa ubora na usalama wa bidhaa nchini na hasa udhibiti wa usalama wa chakula na vipodozi.

Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora wa TBS, Lazaro Msasalaga, alisema kwa miaka mingi tangu kuanzishwa kwa mifumo hiyo ya uthibiti ubora na hadi kufikia mwaka jana (2022), hafla za utoaji leseni na vyeti zilikuwa zinafanyika makao makuu Dar es Salaam.

"Kwa utaratibu huu wazalishaji walilazimika kusafiri kutoka mikoa yao hadi Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki hafla hizi. Hata hivyo, utaratibu huu uliwafanya wengi washindwe kushiriki kwa sababu mbalimbali ikiwemo umbali na gharama, lakini sasa tumeanza kusherehekea utoaji wa leseni na vyeti kikanda," alisema Msasalaga

Alisema hatua hiyo inatokana na kukamilika kuanzishwa kwa ofisi saba za kanda yaani Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam, Pwani na Morogoro); Kanda ya Kati (Dodoma, Singida na Tabora); Kanda ya Kusini (Mtwara, Lindi na Ruvuma); Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya, Songwe, Iringa na Njombe); Kanda ya Magharibi (Kigoma, Katavi na Rukwa); Kanda ya Ziwa (Mwanza, Shinyanga, Geita, Mara, Simiyu, Kagera) na Kanda ya Kaskazini (Arusha, Manyara, Kilimanjaro, Tanga).

"Tunapenda kumshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwezesha uanzishwaji wa kanda kwa kuidhinisha Muundo Mpya wa TBS Desemba, 2021, muundo ambao umewezesha uanzishaji wa kanda hizi," alisema.

Alisema sambamba na uanzishwaji wa ofisi za kanda, Mpango Mkakati wa TBS umejielekeza katika ujenzi wa maabara katika kila kanda ili kuhakikisha kuwa huduma zote za upokeaji na uchakataji maombi, ukaguzi wa viwanda, upimaji wa sampuli na utoaji leseni na vyeti unafanyika katika kanda ili kuunga mkono juhudi za Serikali katika kusogeza huduma kwa wananchi na kuboresha mazingira ya biashara nchini.





# Serikali yaahidi kutenga fedha ujenzi vituo afya

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imesema itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye Kata za kimkakati nchini zikiwamo Mnongodi na Nyundo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Deogratius Ndejembi, alisema hayo jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji ni lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa vituo vya afya katika Kata za Mnongodi na Nyundo.

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali ilitenga Sh.bilioni 117 kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya vya kimkakati kwenye Kata 234.

"Halmashauri ya Mji wa Nanyamba ilitengewa kiasi cha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kitaya ambacho ujenzi wake upo hatua ya ukamilishaji," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji kutokana na ujenzi wa kituo cha Kitaya kukamilika lini serikali itapeleka vifaa tiba na wataalamu ili huduma zitolewe.

"Je, serikali katika bajeti ya TAMISEMI iliyopitishwa ya ujenzi wa vituo vipya vya afya, inatoa tamko gani ujenzi wa vituo vya afya kata za kimkakati jimbo la Nanyamba?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema katika mwaka 2023/24 serikali imetenga Sh.milioni 400 kwa ajili ya ununuzi vifaa tiba vya zahanati na vituo vya afya kwenye mji huo.

Hata hivyo, alisema serikali itahakikisha inatenga fedha za vituo vya afya vya Nanyamba.

# USAID yatoa Dola milioni 12 kusaidia vijana sekta kilimo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Marekani (USAID) limetoa zaidi ya Dola za Kimarekani milioni 12 ili kuimarisha ujasiri wa vijana katika sekta za kilimo.

Mkurugenzi Mkazi wa USAID Tanzania, Kate Somvongsiri, aliyasema hayo juzi jijini hapa, kwenye hafla ya uzinduzi wa mradi wa Feed The Future wenye lengo la kuimarisha sekta binafsi (PSSA).

Alisema katika kutekeleza programu ya PSSA itaambatana na kuunga mkono Mpango wa Wizara ya Kilimo wa Kujenga Kesho Bora (BBT).

"Kwa kufanya hivyo PSSA itawafikia vijana 30,000, kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa angalau makampuni 3,000 yanayoongozwa na vijana,"alisema.

Aidha, alisema shughuli ya kuimarisha sekta binafsi ya Feed The Future Tanzania itatoa ruzuku kwa vyama vya wafanyakazi binafsi, mashirika na kampuni kubwa ambazo zitaboresha mazingira wezeshi ya biashara na kupanua fursa za kiuchumi kwa vijana.

"Kwa mfano Khebhandza Marketing Company Limited inapokea ruzuku ya Sh. milioni 287.457 kusaidia kuanzisha kampuni 700 zinazoongozwa na vijana zinazofanya kazi katika sekta ya nafaka, kunde na mbegu za mafuta katika Mkoa wa Mbeya na kuunganisha kampuni hizi na fedha, huduma na masoko,"alisema.

Pia, alisema Jumuiya ya wafanyabiashara Wanawake Tanzania inapokea ruzuku ya Sh. milioni 297.82 ili kuanzisha vituo vya biashara, vinavyounganisha biashara za vijana na utaalam wa kiufundi, huduma za biashara na masoko ya fedha.

Alisema kuwa serikali ya Marekani itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuwezesha wananchi wake kufikia uchumi wa kati.

Kijana Pendo Ndumbaro ambaye ni mmiliki wa Kampuni ya Prano Investment ya mkoani Iringa alisema bado wanakabiliwa na kero mbalimbali ikiwamo mlundikano wa kodi.

"Changamoto nyingine ni vifaa duni kwa ajili ya kuzalishia bidhaa mbalimbali, na hii inatokana na ukosefu wa mitaji kwa vijana wafanyabiashara,"alisema.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Dk. Hussein Omary alisema serikali inatambua umuhimu wa sekta binafsi katika kukuza kilimo.

"Tunaishukuru sana serikali ya Marekani kupitia shirika lake la USAID, mradi huu utasaidia kuwezesha vijana kupata mitaji ambayo imekuwa kilio chao cha muda mrefu nchini,"alisema



Watoto Elisha Osena (kushoto) na Ester Osena wakiwa wamesimama wakati Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (hayupo pichani), akiwatambulisha Bungeni jijini Dododma jana. Mtoto Elisha, alikuwa mgonjwa wa selimundu na alipandikizwa uloto kwa msaada wa mdogo wake Ester alipokuwa akipata matibabu katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, ambapo ugonjwa huo umeanza kutibiwa nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH.**

# Wasiokatisha tiketi za kielektroniki waonywa

**Na Thobias Mwanakatwe, SINGIDA**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), Mkoa wa Singida, imewaonya mawakala wa mabasi ya abiria wanaokatisha tiketi ambazo siyo za kielektroniki katika vituo visivyo rasmi kutokana na kuikosesha serikali mapato.

Ofisa Kodi wa TRA, Hashim Mkwayu, alitoa onyo hilo jana alipokuwa akitoa elimu kuhusu kampeni ya Tuwajibike yenye lengo la kuwataka wafanyabiashara na mawakala wa mabasi kutoa risiti za kielektroniki (EFD) wanapouza bidhaa zao.

Akiwa kituo kikuu cha mabasi Misuna, alisema TRA haitasita kuwachukulia hatua kali za kisheria mawakala hao watakaobainika kutotoa tiketi ambazo siyo za kielekroniki kwa abiria na abiria ambaye atashindwa kudai tiketi za EFD.

Mkwayu alisema adhabu hiyo pia, itawahusu mawakala ambao watashindwa kutoa risiti kwa mizigo yote itakayokuwa inasafirishwa kwenye magari hayo.

Alisema kampeni ya Tuwajibike imelenga utoaji wa elimu kwa mawakala wa mabasi kuhusu umuhimu wa kutoa tiketi za kielektroniki kwa abiria na kuwahimiza abiria wao kuhakikisha wanadai tiketi tofauti na hapo watatozwa faini.

Mkwayu alisema kampeni hiyo itawahusu wafanyabiashara wote wenye maduka yanayouza bidhaa mbalimbali, maduka ya dawa, vipodozi, chakula, wauza nyama (bucha) mahoteli, nyumba za kulala wageni, vifaa vya ujenzi nguo na nyingine zote.

Alisema wameamua kufanya hivyo kutokana na kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa baadhi ya mawakala hao kuhusu kuwapo kwa vituo bubu ambavyo vinasababisha mkanganyiko wa bei. Ofisa Elimu kwa Mlipakodi TRA Mkoa Singida, Swaumu Mvungi, alisema mamlaka hiyo itaanza kuyafuatilia maeneo yote ambayo sio rasmi yanayotumika kama vituo vya magari na kutoa risiti ambazo sio za kielekitroniki.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Mabasi Mkoa wa Singida, Musafiri Ramadhani, alisema jambo la kuondoa vituo bubu liangaliwe kwa mapana kwa kuwa ni tatizo kubwa kwao.

Wakala wa mabasi, Ibrahimu Abdul, alisema vituo bubu vimekuwa ni tatizo kubwa kwao na kuomba vyombo husika ikiwamo Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), TRA, Jeshi la Polisi na Manispaa ya Singida wakae pamoja kutafuta njia ya kuiondoa.





## Mwinyi awapa somo wauguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi, amewataka wauguzi na watoa huduma katika sekta ya afya kuwa na moyo wa huruma, kutumia lugha nzuri na kufuata maadili ya taaluma yao wakati wote wanapotoa huduma kwa wagonjwa.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana katika maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani yaliyofanyika katika ukumbi wa Sheikh, Idrissa Abdul Wakil, Kikwajuni, Zanzibar.

Aliwataka watumishi wote wa sekta ya afya kuendelea kuisaidia serikali katika kutekeleza malengo yake ya kuwapatia huduma bora za afya wananchi wa Zanzibar bila ubaguzi.

Rais Mwinyi alisema serikali yake imefanya jitihada kubwa katika kuongeza bajeti ya sekta ya afya, kujenga miundombinu ikiwamo ujenzi wa hospitali za wilaya na mikoa pamoja na kuzifanyia matengenezo makubwa hospitali na vituo vya afya Unguja na Pemba.

Pia alisema SMZ inaendelea na juhudi katika ununuzi wa vifaa vya kisasa vya uchunguzi na vya tiba sambamba na kuongeza nafasi za ajira kwa madaktari na watumishi wingine wa afya Pamoja na kuendeleza mpango wa mafunzo ili kuwajengea uwezo watumishi wa sekta hiyo ili kuongeza ufanisi.

"Hapana shaka kwamba bila wauguzi kutekeleza vyema majukumu yao, afya ya jamii na maisha yao kwa jumla yako mashakani," alisema.

Aliwapongeza wauguzi ambao wanafanya kazi vizuri kwa uadilifu na kujituma usiku na mchana bila kuchoka ya kuhudumia wagonjwa na kuwasihi kuendelea na kuwa na moyo huo ili kufanikisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Akizungumzia changamoto zinazowakabili katika kazi yao zikiwamo uhaba wa wauguzi, alisema serikali kupitia Wizara ya Afya imeanza kuajiri watumishi wa kada hiyo na itaendelea kufanya hivyo katika mwaka ujao wa fedha.

Dk Mwinyi aliiagiza Wizara ya Afya kuhakikisha inatoa fursa za masomo za ndani na nje ya nchi kwa kada hiyo na kuhakikisha wanayatafutia ufumbuzi wa haraka changamoto ya kukosa posho ya dhamana na sare kwa watumishi hao. Mwenyekiti wa Jumuiya za Wauguzi Zanzibar (ZANA), Dk. Rukia Rajab, alisema pamoja na kada hiyo kukabiliwa na changamoto mbalimbali, wasikate tamaa bali wazibadilishe kuwa fursa na chachu ya kufanya kazi na kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa kwa kuwahudumia wagonjwa wenye uhitaji na jamii kwa ujumla.

Aliwataka wauguzi na wakunga wa Zanzibar kunatoa huduma bora kwa wagonjwa kwa kuzingatia maadili na utendaji uliotukuka ili kuimarisha afya za jamii na kuisaidia serikali katika kufikia malengo endelevu ifikapo mwaka 2030.

# Maambukizi VVU yaongezeka visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, amesema ugonjwa wa Ukimwi upo Zanzibar na hadi Desemba, mwaka jana, watu 8,975 walisajiliwa katika kliniki za tiba.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2023/24.

Harusi alisema mwaka jana wakati akiwasilisha makadirio ya wizara hiyo, watu waliosajiliwa walikuwa 7,589.

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kwamba kuna ongezeko la watu 1,386 na uzito wa maradhi unaendelea kuwaelemea wanawake kuliko wanaume.

Waziri alisema kati ya watu 8,975 walioambukizwa virusi vya Ukimwi (VVU, watu 6,074 ni wanawake sawa na asilimia 67.6 wakati wanaume ni 2,901, sawa na asilimia 32.3.

"Ili kukabiliana na hali hii, nachukua fursa hii kuziomba taasisi za serikali na zisizo za kiserikali kushiriki kikamilifu katika kuchukua hatua zitakazosaidia kulimaliza tatizo hili ndani ya visiwa vyetu ifikapo mwaka 2030," alisema.

Waziri huyo alisema katika kipindi cha mwaka 2022/23, Tanzania imefanya tena utafiti wa kuangalia vishiria vya matokeo kwa masuala ya VVU na Ukimwi (Tanzania HIV Impact Survey - THIS).

Alisema Tume ya Ukimwi Zanzibar kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi ya Tanzania Bara na washirika wa maendeleo ilishiriki kikamilifu katika kufanikisha utafiti huo.

"Matokeo ya utafiti yatasaidia kutuonyesha picha halisi ya wapi tumefika kitaifa katika mapambano dhidi ya Ukimwi na kusaidia katika kuandaa mipango madhubuti katika kukabiliana na tatizo hili," alisema. Pia alisema wizara yake kupitia Tume ya Ukimwi inaendelea kutoa taarifa na elimu za VVU na Ukimwi ili kuongeza uelewa juu ya masuala hayo kupitia mikutano, mabonanza, matukio mbalimbali ya kitaifa.

Hata hivyo, alisema wizara yake imefanya mikutano ya uratibu iliyojumuisha wadau wa sekta za Serikali na asasi za kiraia kwa lengo la kuimarisha huduma za afya ya uzazi, katika vituo vya tiba na vituo vya huduma rafiki kwa vijana.

Alisema watu 6,412 walipima hadi Septemba 2022 na kati yao, watu 318 waligundulika kuwa na maambuzi wakiwamo wanaume 244 na wanawake 74.

Waziri huyo alisema pia jumla ya watu 368 walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa shingo ya kizazi na 24 waligundulika na tatizo hilo katika kliniki za tiba.

Wajumbe wa baraza hilo waliochangia makadirio hayo, waliitaka wizara kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo ili kutokomeza maambukizi mapya ya virusi hivyo.




Baadhi ya waunguzi wakiandamana na mabango yenye ujumbe mbalimbali, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani katika viwanja vya Ukumbi Idrisa Abdulwakil Kikwajuni, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Zanzibar yajivunia mafanikio mapambano dawa za kulevya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (smz) imepata mafanikio makubwa katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya kupambana na dawa hizo.

Katika mapambano hayo, watuhumiwa 15 wametiwa hatiani na kuhukumiwa adhabu mbalimbali vikiwamo vifungo vya maisha.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema hayo jana wakati akiwasilisha makadirio mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje kidogo ya mji wa Zanzibar.

Alisema mafanikio hayo yametonana na serikali kuwasilisha muswada wa marekebisho ya kuanzishwa kwa sheria ya kuundwa kwa mamlaka kamili ya kudhibiti na kupambana dawa za kulevya sheria namba 8 ya mwaka 2021 ambayo imepewa mamlaka kamili ya kushughulikia suala hilo.

Kwa mujibu wa Waziri, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imepewa mamlaka kamili ikiwamo kukamata na kuendesha kesi mahakamani hatua ambyao imetoa matokeo mazuri ikiwamo kesi za watuhumiwa kusikilizwa na kutolewa uamuzi haraka.

Pia alisema kituo cha kurekebisha tabia kwa watu walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya kinaendelea vizuri kutoa huduma huko Kidimni wilaya ya Kati Unguja.

"Kituo hicho kinawapatia ujuzi vijana walioathirika na matumizi ya dawa za kulevya ili kuwasaidia katika kujishughulisha na kazi za kuwaingizia kipato," alisema.



**DRAKE**
UKURASA 14

Nipashe BT
JUMAMOSI MEI 13, 2023



# TUWAACHE WALALE

Staa wa muziki wa Bongo fleva, Marioo ameweka wazi kuwa uhusiano wake wa kimapenzi na binti wa Kajala Masanja, Paula wala siyo kiki bali ni uhalisia.

Marioo amelisimulia penzi lake na Kajala kwa hisia kali sana, akisema yaani binti anapotabasamu kwake hoi, na akila akifanya hivyo anamuona kama ndiyo kwanza wanaanza uhusiano.

"Penzi langu na Paula siyo kiki, unajua mi siyo muongo muongo, ukweli ndiyo unasimama hapo hapo. Nafikiri muda sasa unaruhusu, watu walishaanza kunihisi vibaya unajua, nampenda kwa sababu imetokea hisia zimeendana.

Unajua jinsi ilivyo yule mtoto kila anapotabasamu, yaani namuona kama mpya, yaani nampenda sana. Kwenye simu yangu nimemsevu 'For Life'. Tuna ndoto kubwa sana, hatujaoana, lakini yeye ni mwanamke wangu na mimi ni mwanaume wake." Anaongea Marioo kwa hisia kali.

Kuhusu kama penzi hilo limepata baraka kutoka kwa wakubwa, Marioo akasema mama yake Paula, Kakala Masanja anaheshimu sana uhusiano huo na pia akimuona binti yake yupo kwenye kilele cha furaha.

"Hata mama (Kajala) ameheshimu kumuona binti yake yuko kwenye furaha kubwa sana na imefika kwenye kiwango cha juu sana."

Halafu Marioo kama kawaida akaendea kuweka wazi hisia kali za kimapenzi juu ya binti huyo mrembo.

"Kusema kweli nilikuwa sijawahi kupenda kama ninavyompenda huyu mwanamke, sikuwahi kuwa na hii hisia niliyokuwa nayo sasa hivi, ndiyo maana nashindwa kuikabili kabisa," alisema.

Inawezekana Marioo amepunguza kabisa machungu aliyoyapata baada ya kuachana na aliyekuwa mpenzi wake msanii Mimi Mars.

Haya sasa vijana ndiyo hao wamependana, nilishe nikulishe, vizabizabina jifungieni ndani, watu waache kuwapigia kelele, waacheni walale.

BASI SAWA

## Sholo Mwamba usela sasa basi

“Sisi kwetu kwenye muziki wa singeli, hakuna anayeweza kusimama pale mbele akaonekana kama kioo, kwenye bongo fleva au hip hop wapo, wanamuziki wanzangu wajue kuwa sasa huu ni wakati mwingine muziki ni biashara bila ya kushirikiana hatutofika.



Tunatakiwa kuwa na dira ya mtu ambaye ni kioo. Iwe mtu kama Sholo Mwamba ametoka mtaani, amepambana kwa sasa ni staa na ana magari na mali, kwa sisi hakuna.

Ndiyo maana unaniona mimi hapa kama Sholo Mwamba sasa hivi napambana kutoka kwenye maisha ya kisela kuja kwenye maisha mengine. Kwa sasa tunapata sapoti kutoka serikali, imekuwa ikituamini na kutuchukua wakati mwingine kwenye matamasha, wakati mwingine unataka kusafiri, sasa unakuwa unaongea au kufanya mambo yasiyo na maana, Baraza la Sanaa, Basata atakuuliza wewe si uliongea maneno haya? Utajibu vipi?

## ‘Cover Deluxe Edition’ ya Marioo hii hapa

Msanii Marioo ameamua kutambulisha cover ya ngoma zake nne kwenye ‘Deluxe Edition’ ya albumu yake ya ‘The Kid You.’



Ngoma zilizotambulishwa kwenye ‘cover’ hiyo ni ‘Nikazama’, ‘Sing’, ‘Tomorrow’, na ‘Tunamjua.’

Tayari alishatoa ngoma 17 kwenye albamu yake hiyo, hivyo ameongeza nne za ziada na kufikisha pini 21 sasa.

Miezi kadhaa iliyopita ilitoa albamu hiyo na zote hizo alitarajia kuzitangaza jana rasmi kwenye ukumbi wa Werehouse Masaki, Dar es Salaam.

Katika album hiyo amewashirikisha wasanii kibao, akiwemo Alikiba, Harmonize,



# HARMONIZE YASIJE YAKAWA YA KAJALA!

STAA wa muziki wa bongo fleva, Harmonize ameingia tena kwenye mahusiano mengine baada ya kubwagana na Kajala Masanja kuachana katikati ya Desemba mwaka jana.

Safari hii kaopoa ngoma kutoka Rwanda. Demu wake mpya anaitwa Phiona. Mwenyewe amethibitisha hilo kupitia inta stori yake, huku akimwagia sifa kedekede. Anasema eti, mlimbwende huyo ni mrembo mno kuliko wanawake wake wote waliopita. Ana maana Ma-Ex wake wote hawampati huyu wa sasa.

Baada ya kuthibitisha hilo, akaposti nyingine akisema yupo tayari kuchora tatto nyingine ya mrembo huyo. Akashusha sasa sifa kwa mrembo wake mpya Phiona kuwa ana sura na muonekano mzuri na itakuwa vema kama ataichoma sura ya mrembo huyo kwenye mwili wake.

Harnonize amewahi kuwa na wapenzi kadhaa, lakini anayejulikana zaidi ni Kajala ambaye walikuwa na mahusiano kwenye vipindi viwili tofauti.



# Aslay kumbe Chakudeka

MSANII Aslay Isihaka ameibuka na albamu yake mpya inayoitwa ‘Chakudeka’, ambayo imeshaanza kufanya vema mitandaoni na kwenye vyombo mbalimbali vinavyopiga muziki wa bongo fleva.

Aslay, zao ya bendi ya Yamoto, iliyovuma enzi hizo amefyatua albamu hiyo Mei 5, ikiwa na ngoma 10 zote kali ambazo tayari mashabiki wameanza kuzipambanisha zenyewe kwa zenyewe, kusaka kali zaidi kuliko nyingine.

Ngoma zilizo ndani ya albamu hiyo ya kwanza ni ile inayobeba jina, ‘Chakudeka’, ‘Nimenasia’, Arejee,’ 4 Mnafiki,’, na ‘Romantic.’ Zingine ni ‘Sikuachi’, ‘Mama Yoyoo’, ‘Kangaroo’, ‘Nyuki’, na ‘Nice Couple.’

Hata hivyo albamu hiyo ameitoa kwenye mfumo wa audio, huku akiwa kwenye harakati ya kuzitoa ngoma hizo kwa mfumo wa video siku si nyingi.

Aslay aliyejitoa Yamoto Band mwaka mwishoni mwa 2016, alisema kunvunjika kwa kundi hilo kila mtu kutaka kutamani kufanya kazi peke yake na hiyo ni baada ya mashabiki kuanza kuwasifia kila mmoja kivyake na kuanza kuwashindanisha.

# WANYAMA WA BONGO FLEVA

**Na Adam Fungamwango**

MUZIKI una mambo mengi sana, na wanamuziki pamoja na wasanii pia wana mambo mengi pia. Ili kuwa maarufu wanamuziki na wasanii hupitia changamoto mbalimbali, kubwa na ndogo hadi kuupata ustaa. Mara nyingi wanapoupata na kujulikana na wasanii hupewa au kujipachika majina mbalimbali, yanayoakisi kile wanachokifanya au kupitia wakati wa changamoto.

Mfano kwenye muziki wa dansi, wanamuziki wengi walijipachika au kupachikwa majina ya ndege. Hii tutaizungumzia wiki ijayo kwenye safu hii hii.

Leo tuwaangalie wasanii wa muziki wa kizazi kipya. Hawa wengi wao wamepewa au kujipa majina ya wanyama. Hebu tuwaangalie na tabia za wanyama ambazo wamejipa majina yao.

**Diamond Platnumz-Simba**

Hili jina lilikuwa linatumiwa zamani na Afande Sele. Lakini kwa sasa limechukuliwa na mwanamuziki nyota kwa sasa, si Tanzania tu, bali Afrika nzima kama si dunia nzima. Yeye anaitwa simba.

Kama inavyofamika na wengi kuwa mnyama simba ambaye ni jamii ya paka, ndiye mfalme wa mwituni. Siyo mkubwa kuliko wanyama wote, ila ni mnyama anayeogopwa na wanyama wote mwituni, wakubwa na wadogo.

Sababu kubwa si kwamba ana nguvu sana kuliko wote, bali anatumia nguvu alizonazo akichanganya na akili, ujanja na mbinu nyingi ambazo wanyama wengine hawana. Ndiyo maan anaitwa mfalme wa wanyama pori wote.

**Harmonize-Tembo**



Msanii Harmonize, yeye anaitwa tembo. ameitwa au kujiita hivyo nadhani si kwa ajili ya mwili wake mkubwa, bali uwezo wake wa uimbaji ni mkubwa akijifananisha na mnyama huyo.

Ikumbukwe kuwa tembo ni mnyama mkubwa zaidi na ana uzito mkubwa kuliko Simba.

Simba mwenyewe hawezi kumkamata tembo mkubwa, labla mtoto wake. Tembo hali nyama, majina ya wasanii wengine walijipa majina ya wanyama wala wenzao.

Lakini ukweli unabaki pale pale kuwa tembo ni mkubwa kuliko wanyama wote porini, lakini anazidiwa na simba kwenye ufundi, ujanja, na mbinu ambazo mfalme wa wanyamapori amebarikiwa.

**Rayvanny-Chui**

Msanii mwingine mwenye sauti nyororo, Rayvanny, yeye anajiita chui. Huyu naye ni jamii ya paka. Muonekanano wake kama paka mkubwa au simba jike. Lakini ana madoadoa. Sifa yake ni tofauti kidogo na simba. Pamoja na kwamba wote wanawinda wanyama, lakini chui yeye kwanza anapenda kukaa juu ya miti, tofauti na simba.

Huyu ana hasira zaidi ya kujeruhi na kukishambulia chochote kile anachokiona, tofauti na simba ambao yeye hafanyi hivyo bila sababu yoyote. Naye ana sababu zake za kujiita chui.

**Country Boy-Fisi**

Ni msanii kutoka Konde Music Worldwide. Yeye naye akaamua kujiita fisi. Ni mnyama ambaye anakula wanyama au ndege waliokufa. Kuna wakati anawinda mwenyewe, ila hana tatizo kula mnyama au ndege au amemkuta ameshafariki, maarufu mama mizoga, tofauti na simba ambaye ni lazima akamate mwenyewe kitoweo ndiyo ale.

Mwenyewe anadai anajiita jina hilo kutokana na tabia za mnyama huyo ambazo zinashabihiana na mwenendo wake katika muziki.

**Dudubaya-Mamba**

Msanii mkongwe kabisa, ambaye ni mmoja kati ya waanzilishi wa muziki wa bongo fleva mwanzoni mwa miaka ya 2000. Dudubaya yeye akajiita mamba. ni Mnyama anayeishi majini, kwenye mito, maziwa na ardhi tepetepe na yeye hula nyama pia.

FILAMU

# Binamu: Mzaha mzaha hutumbuka usaha

**Na Adam Fungamwango**

PENZI halichezewi na wala halijaribiwi. Ndivyo unavyoweza kusema. Ni msemo wa wahenga tangu enzi na enzi. ‘Binamu’ ni filamu iliyochezwa na wasanii Affan Jamal, Diana James, Ahur James, Jumanne Simba na wengine. Ni filamu inayotoa funzo watu kuwa waangalifu sana wanapokuwa kwenye mahusiano au ndoa.

Usimfanyie kitu mpenzi wako ambacho wewe hutaki kufanyiwa. Kwa sababu ipo siku utakuja kufanyiwa wewe ukakasirika.

Jamaa mmoja anaitwa Sharukhan. Huyu ana mkewe Zaina. Kwa sababu wamekaa muda mrefu bila ya kuwa na mtoto, Sharukhan anamwambia mkewe amelete dada yake binamu ili angalau nyumba ichangamke. Analetwa dada mmoja anaitwa Ashura. Ni Ashura, Ashura kweli. Kipande cha dada, kimeumbika.

Siku si nyingi, mke wa Sharukhan akaanza kuona kama mwenendo wao siyo mzuri. Walionekana ni kama wapenzi hivi. Mara kwa mara akawa wanawakuta wanadekezana na kukumbatiana. Zaina anapoulizwa akaambiwa kuwa hiyo ndiyo tabia yao tangu utotoni kwa sababu wamekuwa pamoja.

Hali hiyo ilimfanya Zaina asipate usingizi. Akawaza na kuwazua. Iko siku na yeye akakata shauri ya kumpigia kaka yake binamu aje. Sharukhan akafungwa kamba kuwa kaka wa mkewe anakuja kusalimia. Lakini lengo ilikuwa ni kulipiza kisasi.

Anakuja kaka yake. Kinachotokea ni kama kile ambacho Sharukhan na Ashura wanafanya. majirani wanaona kila kitu. Na kwa bahati nzuri au mbaya, Zaina na kaka yake wanacheza ngoma, kuimba na kukumbatiana hadharani. Sharukhan anaambiwa yote. Mapenzi yanauma. Hali ya jamaa ilianza kubadilika. Sasa hata dada yake binamu, akitaka kudekezane, Sharukhan hataki. Akili yote ni kwa mkewe akiona kabisa sasa anaibiwa.

Akaitisha kikao. Akaanza kutoa kilicho moyoni mwake. Mkewe akasema amefanya vile kwa sababu ya kulipa kisasi cha kile ambacho anafanyiwa ndani ya nyumba hiyo.

Alivyoona haelewi, maana Ashara dada si dada, basi akaona na yeye akamlete kaka yake binamu kwa ajili ya kuigiza kama wanavyofanya mumewe na Ashura ili kuweka mambo sawa. Akamwambia mumewe kuwa hata yeye alikuwa anaumia sana kwa alivyokuwa anafanyiwa.

Mwisho wa siku, kaka binamu wa Zaina ilibidi arudishwe kwao, Ashura akatafutiwa mchumba ambaye ni rafiki wa Sharukhan, yeye mwenyewe akabaki na mkewe.





# Du! Kumbe Drake Mnigeria bwana!

Imedaiwa kuwa rapa wa muziki kutoka nchini Canada, Drake ana asili ya Nigeria.

Hilo limetokea wakati tovuti moja nchini Marekani kuposti na kuuliza watu uasili wa nchi anayotokea rapa huyo mwenye asili ya Afrika.

Asilimia 30 imepiga kura na kusema kuwa Drake ana asili ya Nigeria taifa ambalo lipo Afrika. Asilimia 28 ya waliopiga wakasema ana asili ya nchi za Cameroon na wengine Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Mchakato wa upigaji kura huo na matokeo yake, yalionekana kumkuna Drake mwenyewe, akaamua kuposti kwenye insta stori yake.

Na yeye akaamua kuuliwa kuwa inawezekana baba yake akawa raia wa Nigeria? Nadhani wapiga kura wale wale wanaweza kumjibu.




## Lil Wayne kila ngoma yake

Lil Wayne amekiri kwamba mafanikio yake makubwa kimuziki ilikuwa mwaka mwaka 2007 alishirikishwa kwenye ngoma zaidi ya 100, kiasi ambacho akiwasha redio kwenye gari lake, redio yoyote ikiwekwa basi lazima akutane na sauti yake!

Jamaa alifunguka kwenye mahojiano kwenye kipindi kimoja cha nchini Marekani. Akasema mwaka 2007 na 2008, alifikia kuwa kama rapper mkuu kwani Albamu yake ya mwaka ya 2008 ya Tha Carter III, ilibaki kuwa kenye chati ya Billboard 200 kwa wiki tatu mfululizo. Lakini mwaka mmoja kabla ya hapo, Wayne alisema alikuwa na ngoma nyingi akishirikiana na karibu kila wimbo maarufu wa 2007.

Mnamo 2007, alikuwa na ngoma sita alizoshirikishwa kwenye 'the Land 100', ambazo zilijumuisha nyimbo 15 bora kama vile 'Sweetest Girl (Dollar Bill) ya Wyclef Jean, iliyoshika namba 12 na 'Duffle Bag Boy', ya Playaz Circle iliyoshika Namba 15.

## DJ Maphorisa demu hapigwi makofi

Wabongo wana msemo wao kuwa msemo unaosema 'mwanamke hapigwi kwa fimbo au makofi, hupigwa na upande wa khanga', lakini hiyo si kwa mtayarishaji wa muziki wa Amapiano nchini Afrika Kusini, Themba Sekowe, maarufu kwa jina la DJ Maphorisa.

Yeye akamlamba makofi mpenzi wake Thuli Phongolo, na kumpa kipondo cha nguvu kiasi mpaka askari wakaenda kumkamata. Kwa mujibu wa habari kutoka kwenye magazeti na mitandao mbalimbali ya Sauzi, kisa hicho kimetokea wiki hii, ambapo demu wake ambaye ni mwigizaji alifungua kesi ya tukio hilo katika taarifa iliyoonekana kwenye machapisho.

"Nilimkabili ili tuzungumze kuhusu mabishano yetu yaliyotokea usiku uliopita wakati wa tafrija yake, lakini alinishika shingoni kwa fujo, akinishambulia,' Thuli alisema kama alivyonukuliwa.





## Mgonjwa Foxx sasa anakunywa uji

Mgonjwa mwingizaji Jamie Foxx ambaye ambaye ameripotiwa kuwa yuko hoi hispitalini, hali yake sasa inatia matumaini na kwa kiswahili cha Kibongo tunaweza kusema kuwa 'mgonjwa anakunywa uji.'

Wabongo wanatumia msemo huu kuashiria kuwa yoyote yule ambaye ni mgonjwa awe nyumbani au amelazwa hospitalini, anaendelea vizuri na anatia matumaini na afya yake imeendelea kuimarika.

Mgonjwa akawatoa wasiwasi wafuasi na mashabiki wake kwa kuandika kwenye mtandao yake ya instagram maneno yafuatayo.

"Nathamini upendo wenu wote, na hajisikia kubarikiwa." Akaandika mwenyewe na kuwashusha presha mashabiki.

Awali kulikuwa na maneno mengi mitandaoni kufuatia hali ya kiafya ya mwigizaji huyo.

Mnamo Aprili, familia yake ilifichua kwenye Instagram kwamba mwigizaji huyo aliugua na kukimbizwa hospitalini na hii ni kutokana na chapisho lililoshirikiwa na binti yake Corinne, ambalo lakini aliliondoa baadaye. Amba-

## Ed Sheeran chupuchupu kulipa Sh bilioni 230

Mahakama ya Manhattan, New York nchini Marekani imesema mwanamuziki Ed Sheeran alitunga na kutengeneza wimbo wake kwa kujitegemea yeye mwenyewe na hakuna kipengele chochote kwenye utunzi wa nyimbo hiyo kilichotoka kwenye wimbo wa Marvin Gaye aliyefariki mwaka 1984.

Kesi hii ilikamata vichwa vya habari duniani baada ya mashtaka hayo dhidi ya Ed Sheeran kufunguliwa mwaka 2017 ila hatimaye uamuzi ulitolewa mwaka huu kuhusu sakata hili ambalo mshtakiwa aliwahi kuweka ahadi ya kuacha kufanya muziki endapo angekutwa na hatia ya kuiba wimbo wa Marvin Gaye.

Ndugu wa mtunzi mwenza wa wimbo wa Marvin Gaye walimfungulia kesi Sheeran wakidai kwamba mdundo wa sauti wa nyimbo hizo mbili ulikuwa unafanana wakisema Ed Sheeran alikiuka hakimiliki.





Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Edmund Rutaraka (wa pili kushoto), akionya kuhusu uharibifu wa mazingira katika vyanzo saba vya maji wilayani humo, baada ya kamati ndogo iliyoundwa kuchunguza hali hiyo kuwasilisha ripoti yake katika kikao cha Baraza la Madiwani juzi. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Matukio 2,347 ukatili kijinsia yaripotiwa siku 90 Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

UKATILI wa kijinsia katika mkoa wa Manyara, umeendelea kuwa tishio, baada ya serikali kuthibitisha kutokea kwa matukio 2,347 katika kipindi kisichozidi siku 90.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Manyara, Lilian Bujune, alisema jana kuwa, waathirika wakuu wa vitendo hivyo ni watoto wenye umri wa miaka miwili hadi minane pamoja na wanawake.

"Kati ya Januari na Machi, mwaka huu, kumetokea matukio hayo ambayo yameripotiwa kupitia DHIS2 (Mfumo wa Afya wa Wilaya).

"Hali halisi inaonyesha kuna uwezekano mkubwa wa matukio haya kuwa mengi zaidi kuliko namna yalivyoripotiwa, hasa ukizingatia kuwa Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto nchini," alisema.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, ukatili wa kimwili unaohusisha kujeruhi mwili ni matukio 944, ukatili wa kingono unaohusisha ubakaji na ulawiti yako matukio 285 na ukatili wa kiuchumi yako matukio 187.

Sababu za ukatili huo zinatajwa kuwa ni ukimya wa wanajamii matukio yanapotekea, mmomonyoko wa maadili na mfumo mbovu wa malezi na makuzi katika jamii.

Aidha, inaelezwa kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha watoto wengi kukosa walinzi na watu wa karibu wa kuwahudumia, huku uelewa mdogo wa jamii kuhusu ukatili ukitengeneza njia zaidi kutokana na mila na desturi kandamizi.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Karolina Mthapula, akizungumzia hali hiyo, alisema matukio hayo yanasikitisha na hayakubaliki katika jamii iliyostaarabika.

Mthapula alisisitiza kuwa mwaka jana, zaidi ya matukio 3,000 yalitokea kwa kipindi cha Januari hadi Mei, mwaka huu. "Twendeni sasa tujenge urafiki na watoto ili watupe taarifa za ukatili wanaofanyiwa shuleni au maeneo wanakocheza," alisema.

# Mbunge amwangukia Rais malipo ya fidia

**Na Oscar Assenga,** MKINGA

MBUNGE wa Mkinga, mkoani Tanga, Dastan Kitandula (CCM), amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kumsukuma mwekezaji wa kiwanda cha Saruji cha Hengya, kuwalipa fidia ya ardhi wananchi wa vijiji vya Kwale na Mtimbwani waliokubali kupisha mradi mkubwa wa ujenzi wa kiwanda kipya cha saruji.

Wananchi hao wanadai fidia ya zaidi ya Sh. milioni 570 kutoka kwa mwekezaji huyo.

Akizungumzia sakata hilo jana, Kitandula alisema mwaka 2017 mwekezaji huyo alijitokeza na kuonyesha nia ya kuwekeza kiwanda cha saruji.

"Mwaka 2019 TIC (Kituo cha Uwekezaji Tanzania) kilimpa leseni aje awekeze, lakini baada ya kupatiwa leseni mwaka 2020, alianza kulipa fidia ya ardhi aliyoitwaa, cha ajabu mpaka leo, hakuna fidia stahiki iliyoendelea kutolewa.

"Hivi sasa wako wananchi 143 wa Mkinga kutoka Kwale na Mtimbwani wanadai zaidi ya Sh. milioni 570, ambazo bado hazijalipwa," alisema.

Alisema serikali ilituma timu ambayo ilikaa na kukaa na uongozi wa Mkoa na wilaya pamoja na mwekezaji na kukubaliana ifanyike tathimini isiyo na shaka ili watu walipwe na kazi hiyo imekamilika na kupelekea lakini amegoma kulipa viwango stahiki vya kisheria.

Mbunge huyo alisema wananchi wamepoteza ardhi zao kwa muda mrefu na hawana ruhusa ya kuingia kwenye maeneo hayo.

Mwekezaji huyo, amepanga kutumia zaidi ya Sh. trilioni 2.3 kwa ajili ya uwekezaji huo wa kiwanda cha saruji ambacho kikikamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni saba kwa mwaka.

# Wanafunzi 735 waliochaguliwa kidato cha kwanza hawajaripoti

**Na Dege Masoli,** KILINDI

WANAFUNZI 735 waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka huu katika wilaya ya Kilindi mkoani Tanga, hawajaripoti shuleni mpaka sasa.

Taarifa iliyowasilishwa jana katika kikao cha Baraza la Madiwani la Wilaya hiyo na Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, Juma Bewa, inaonyesha kuwa wanafunzi hao ni kati ya watoto 5,037 waliohitimu darasa la saba mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa Bewa, idadi hiyo ambayo ni kubwa kwa wanafunzi kushindwa kuripoti shuleni kutokana na sababu mbalimbali, inaathiri ufaulu katika wilaya hiyo.

Katika taarifa hiyo, Bewa alisema hadi kufikia Machi 31, mwaka huu, wanafunzi walioripoti katika shule walizopangiwa walikuwa ni 4,272 na kati hao, wavulana ni 1,992 na wasichana ni 2,280 ambao ni sawa na asilimia 85.

"Lakini ambao wameripoti shuleni hadi kufikia Machi 31, mwaka huu, ni wavulana 327 na wasichana wakiwa ni 408."

Akitoa ufafanuzi kuhusu wanafunzi waliochaguliwa, Bewa ambaye pia ni Diwani wa Kilindi Asilia, alisema wanafunzi 5,037 wakiwamo wavulana 2,335 na wasichana 2,702, ndio waliochaguliwa kuingia kidato cha kwanza katika shule 22 za Wilaya hiyo.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti huyo alisema kuwa, kwa mwaka wa masomo 2023 , uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la awali, na la kwanza umevuka lengo kwa kufikia asilimia 138.6 kwa watoto wa awali, huku darasa la kwanza wakifikia asilimia 141.8

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Visa vya Majambo kiboko ya watoto 'vikojozi' enzi hizo

Na Adam Fungamwango

ALIVAA manyoya ya mnyama mbega kichwani na mabegani. Alijifunga meno ya ng'ombe chini ya pua na kuonekana kama meno yake yametokeza kwa mbele.

Kifuani alikuwa wazi, lakini kuanzia tumboni alijifunga vitambaa vya khaki, pamoja na mkoba wake kiunoni. Alivaa pensi, lakini juu yake akiwa amejifunga kibwaya. Mkono wa kushoto alibeba kikapu , huku mkono wa kulia akiwa ameshika usinga.

Miguuni akijifunga vitambaa vya rangi nyeupe na khaki, pamoja na njuga ambazo zilikuwa zikilia kila anapopiga hatua.

Hakuna hata mtu mmoja ambaye hadi leo anayeweza kujua sura yake halisi. Siku akiamua kutembea bila kuwa anavyokuwa siku akiwa kwenye biashara zake, hakuna aliyekuwa na uwezo wa kumtambua.Wale walioishi Dar es Salaam hadi miaka ya 1970 mpaka 1980 watakuwa wanamfahamu mtu huyo. Si watoto wala si wakubwa.

Hata waliokuwa wanakwenda Dar es Salaam kutoka mikoani kusalimia ndugu zao, watakuwa wanamfahamu mtu huyo. Kwa kifupi, muonekano wake ulitisha. Anaitwa mzee Majambo.

Alizurura Dar es Salama nzima akiwa anafanya kazi yake kuu ya kuuza karanga.

Kile kikapu ambacho anakishika mkono wa kushoto kilikuwa na karanga.

Aliuza mitaani, akizunguka kila mtaa wa jiji la Dar es Salaam inayoijua wewe, ingawa wakati huo ilikuwa haijapanuka sana.

Ukiachilia mbali kuuza karanga zake mitaani, alikuwa akita pia kwenye mikusanyiko ya watu kama vile kwenye Hospitali kubwa kama Mwanyamala, Amana, na Mnazi Mmoja.

Alifanya hivyo pia kwenye Masoko Makubwa yote yaliyokuwa Dar.

Hakuwa na kificho anapokaribia kufika popote pale, kwani njuga zake hutoa milio kila anapopiga hatua moja.

Watoto wa wakati ule tulitunga na wimbo kabisa kuwa zilia "Majambo nje, Majambo nje." Mdomoni pia alikuwa na filimbi.

Akiuza sana karanga zake hizo. Yaani alifanya biashara kubwa, kwani akinamama walikuwa wakimwita na kununua karanga zake kutokana na vituko na visa vyake.




Picha hii si ya mwenyewe ila inaonyesha taswira au muonekano aliokuwa nao mzee Majambo akiwa kwenye harakati zake za biashara ya kuuza karanga kwenye jiji la Dar es Salaam miaka ya katikati ya 1970, hadi mwishoni mwa miaka ya 1980.

Anakuuzia karanga huku akiimba na na kucheza. Alikuwa na nyimbo nyingi mbalimbali.

Moja mashairi ya nyimbo zake yalichukuliwa na bendi ya Western Jazz na kutengeneza wimbo wa 'Kipulepule cha malombe.'

Mashairi ya wimbo ule ni wa mzee Majambo ambaye zilikuwa moja ya nyimbo zake maarufu anapouzia watu karanga, akiimba na kucheza.

Pamoja na sifa na visa vyake hivyo, alikuwa akiogopewa sana na watoto wadogo ambao walikuwa bado hawajavuka miaka ya 15.

Ni kwa sababu akinamama walimfanya kama ngao ya kutishia watoto watundu, watukutu au wenye matatizo mbalimbali yanayohitaji kurekebishwa.

Kuna watoto ambao walikuwa na tatizo la kukojoa kitandani. Hawa walitishiwa Majambo.

Mtoto yoyote mwenye tabia hii akiambia ukirudia Majambo akija anaambiwa ili amchukue.

Atafanya chini juu aache. Watoto wenye tabia mbaya, ya uchoyo, kukataa kutumwa, au hata kutopenda kula, kiboko yao alikuwa Majambo.

Akiambiwa ngoja Majambo aje, basi kila kitu kitakaa sawa. Ni kwa sababu moja tu. Muonekano wake ulitisha.

Ni kama kwa sasa hivi wanavyoonekana mazombi kwenye filamu mbalimbali.

Na yeye alionekana hivyo. Fikiria kwa mtoto akiona kiumbe kinachofanana vile laivu inakuwaje.

Huwa akipita watoto wengi hujifungia ndani. Hujificha uvunguni au kukimbia eneo husika hadi aondoke. Ni watoto wachache sana ambao walikuwa na uwezo wa kukabiana ana kwa ana na Majambo. Hilo ndilo lililosababisha akinamama kumtumia kama fimbo ya kuwanyoosha watoto wao wanapofanya makosa.

Wala watoto hakutakiwa kuambiwa kuwa anakuja. Wakisikia filimbi na njuga tu, ilitosha kujua ni yeye na kutafuta wapi pa kujificha.

Tena kwa wale ambao walikuwa wanajijua kama tayari wameshafanya makosa kama kukojoa kitandani, kukataa kwenda shule, kutumkwa, kula, walijua kuna hatari inawabili mbele yao.

Hata hivyo walichokuwa wakifaidi watoto kutoka kwa Majambo ni karanga zake tamu.

Akinamama hununua na kuwawekea watoto wao ambao wakati huo wameshakimbia, kujifungia milango au kujificha uvunguni mwa vitanda. Wanapotoka wakati ameondoka huzifaidi karanga zake.

Wateja wa mzee Majambo walikuwa ni kinamama zaidi. Watoto walimuogopa. Wanaume hawakumuamini. Kutokana na staili yake hiyo, akipita mitaani, sokoni, hospitalini, ikajengwa dhana kuwa ni shushushu mkubwa. Ikasemekana kazi yake ni kukusanya taarifa za nini kinaendelea mitaani hasa kwenye jiji kubwa la Dar na kote anakopita na kuzipeleka kwenye ngazi za juu.

Walioishi Dar miaka hiyo ambao kwa sasa wapo jiji hilo, au kwa sasa wapo kwenye mikoa mingine na nje ya nchi na walipata kumshuhudia na visa vyake tofauti tofauti, wanakaribishwa kuchangia mambo, visa na mikasa ambayo ilitokea kipindi hicho cha Majambo.

**Tuma meseji 0716 350534**


Wananchi mbalimbali nchini Sudan wakiwa wamepanga mstari kusubiri kupatiwa msaada wa chakula ambao umekuwa ni changamoto nchini humo baada ya vita kuanza. **PICHA:DW.**

# Wapinzani Sudan wasaini makubaliano kuwalinda raia

**KHARTOUM,** SUDAN

WAPINZANI wanaopigania madaraka nchini Sudan wametia saini makubaliano ya kuwalinda raia na kuhakikisha huduma za msaada wa kiutu zinawafikia wenye uhitaji bila ya vizingiti.

Taarifa ya makubaliano hayo zilitolewa usiku wa kuamkia jana huku wadau mbalimbali wakieleza kuwa ni taarifa za kutia moyo, na kwamba pande zinazozozana zimekubaliana kuwalinda raia na kuhakikisha huduma za msaada wa kiutu zinafika kwenye maeneo yenye uhitaji bila vizingiti.

Licha ya hatua hiyo, pande hizo mbili hazijakubaliana bado kusitisha mapigano wala kutafuta mkataba mpana wa kumaliza vita.

Maofisa wa Marekani waliokaririwa na Shirika la Habari la Associated Press walisema maafikiano ya kumaliza vita ni jambo ambalo bado haliko karibu.

Baada ya wiki nzima ya majadiliano katika mji wa mwambao wa Jeddah nchini Saudi Arabia, kile kilichopatikana ni pande hizo mbili hasimu kutia saini azimio la kuonesha dhamira ya kufanya kazi pamoja ili kupata makubaliano mapya ya kusitisha vita kwa muda mfupi.

Azimio hilo linatilia mkazo umuhimu wa kila upande kusaidia upatikanaji huduma muhimu za kiutu na kuwalinda raia. Pia linatoa mwito wa kurejeshwa huduma ya nishati ya umeme, maji na nyingine muhimu.

Vikosi vya pande hasimu pia vinatakiwa kuondoka kutoka kwenye majengo ya hospitali na kila upande uruhusu kufanyika mazishi ya heshima kwa wale waliopoteza maisha.

Ofisa mmoja wa Marekani anayeshiriki mazungumzo hayo ameliambia shirika la habari la AFP, kuwa azimio hilo siyo la kusitisha vita na badala yake ni dhamira ya kila upande kulinda na kueshimu wajibu wao kwa sheria za kimataifa za utoaji msaada wa kiutu katika uwanja wa mapambano.

"Tunatumai, japo kwa tahadhari, kwamba dhamira yao ya kutia saini nyaraka hii itafungua nafasi itakayowalazimisha kuweka mazingira ya kuingiza mahitaji ya kibinadamu," alisema ofisa huyo wa Marekani ambaye jina lake halikutajwa.

Kwa mujibu wa maofisa wanaohudhuria mazungumzo ya mjini Jeddah, pande mbili hasimu ambazo ni Jeshi la Sudan na Kikosi cha Wanamgambo wenye nguvu cha RSF wangali wana tofauti kubwa juu ya jinsi mzozo unaoendelea unaweza kufikia mwisho.

Inaelezwa kuwa hali hiyo huenda imewafadhaisha wapatanishi kutoka Marekani na Saudi Arabia walioweka lengo la kufikia mkataba wa kusitisha mapigano ndani ya siku kumi za mazungumzo.

Licha ya mafanikio kidogo yalitangazwa kutokea Jeddah, nchini Sudan kwenyewe mapambano yameendelea kuripotiwa kutwa nzima ya jazi na usiku wa kuamkia jana.

Mapigano yaliutikisa mji wa Halfaya, ambao ni lango la kuingia mji mkuu Khartoum. Wakazi wa eneo hilo walisema walisikia milio ya ndege za kivita ikizizima mjini Khartoum na kwenye miji pacha ya Bahri na Omdurman.

Licha ya rapsha hizo taarifa zinaeleza kwamba mapigano ya jana hayakuwa makali ikilinganishwa na ya siku ya Jumatano. Katika hatua nyingine, hapo jana Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa liliandaa mkutano maalum kuhusu machafuko yanayoendelea Sudan.

Mkuu wa haki za binadamu la Umoja wa Mataifa Volker Turk alitumia mkutano huo wa mjini Geneva, kuirai jamii ya kimataifa kutumia njia zote zinazowezeka kuongeza m'binyo kwa pande zinazohasimiana Sudan ili kumaliza machafuko hayo.

Turk alikumbusha kuwa machafuko hayo yamewatumbukiza Wasudan wengi katika mgogoro na mateso.

Alisema mbele ya macho ya umma, pande hasimu hazioneshi hadi sasa utayari wa kusalimu amri ili kumaliza mzozo huo uliozuka ghafla mwezi uliopita.

Mapigano hayo yanatishia kuitumbukiza Sudan kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe ikiwa tayari yamesababisha vifo vya mamia ya watu na kuzusha hali ngumu ya kibinadamu nchini humo.

Makubaliano ya awali ya kusitisha mapigano yalikiukwa kila wakati na kuwaacha raia wakitaabika katikati ya wimbi la hujuma za kila upande.

Miundombinu muhimu kama umeme na mifumo ya maji imelengwa na mashambulizi. Na kwamba upatikanaji chakula umekuwa wa tabu na mfumo wa kutoa matibabu umeparanganyika.

**DW**

# Marekani yaishutumu Afrika ya Kusini

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

BALOZI wa Marekani nchini Afrika Kusini ameishutumu nchi hiyo kwa kuipatia silaha nchi ya Russia kwa siri, tuhuma ambazo zimezua majibu makali kutoka Pretoria.

Balozi Reuben Brigety aliuambia mkutano wa vyombo vya habari jana kuwa, Marekani inaamini kuwa silaha na risasi zilikuwa zimepakiwa kwenye meli ya mizigo ya Russia iliyotia nanga katika kambi ya jeshi la majini mjini Cape Town mwezi Desemba.

"Tuna uhakika kuwa silaha zilipakiwa kwenye meli hiyo, nasema sidanganyi, nina uhakika kuhusu usahihi wa madai hayo," alisema Brigety kupitia kipande cha video ya matamshi hayo kilichorushwa mtandaoni.

"Kuipa silaha kwa Russia kulikofanywa na Afrika Kusini kimsingi ni jambo lisilokubalika," alisema Brigrty.

Licha ya madai hayo ofisi ya Rais Cyril Ramaphosa ilijibu, kwa kusema kwamba "inasikitisha kuwa Brigety amechukua hatua ambayo haionyeshi picha nzuri".

Matamshi hayo yanadhoofisha hali ya mshikamano na ushirikiano kati ya mataifa hayo mawili, msemaji wa Ramaphosa, Vincent Magwenya alisema katika taarifa yake.

"Wakati hakuna ushahidi uliotolewa hadi leo unaounga mkono tuhuma hizo, serikali imepanga kuanzisha uchunguzi huru utakaoongozwa na jaji mstaafu.

Afrika Kusini ilikataa kulaani uvamizi wa Ukraine, ambao kwa kiasi kikubwa umeifanya Moscow itengwe katika jukwaa la kimataifa.

Inaelezwa kuwa nchi hiyo ni nchi yenye nguvu barani afrika ambayo pia ina maadili yenye ushawishi mkubwa katika ushindi wake dhidi ya ubaguzi wa rangi, na kwamba inasema inataka kutoegemea upande wowote, na kuwa kiongozi katika mazungumzo ya kuumaliza mzozo huo.

Lakini wakosoaji wanataja matukio kadhaa ya hivi karibuni kama ushahidi wa kuegemea upande wa Kremlin.

Mapema mwaka huu, Afrika Kusini ilifanya mazoezi ya kijeshi na Russia pamoja na China, na mwezi uliopita ndege ya mizigo ya kijeshi ya Russia iliyowekewa vizuizi ilitua katika kambi ya jeshi la anga usiku wa manane kupeleka kile ambacho mamlaka ya ulinzi ilikieleza kuwa barua ya kidiplomasia.

**VOA**




Naibu Meya wa Jiji la Dodoma, Jamal Ngalya (kulia), akimkabidhi cheti cha pongezi Diwani wa kata ya Chamwino, Jumanne Ngede kwenye kikao cha baraza la madiwani jana, baada ya kata hiyo kuibuka kwa ushindi wa usafi wa mazingira. Wengine ni Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Lucas Venance (kushoto) na Mkurugenzi wa Jiji hilo, Joseph Mafuru. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Watanzania mil. 33 wachanjwa UVIKO- 19

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, amesema hadi Machi, mwaka huu, Watanzania milioni 32.7 sawa na asilimia 53.4 wamekamilisha chanjo ya UVIKO- 19.

Amesema hadi Machi, mwaka huu, dozi milioni 46.8 za chanjo ya ugonjwa huo zimepokewa na kusambazwa na kwamba dozi milioni 39.1 sawa na asilimia 84 zimetumika.

Ummy alisema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Waziri Ummy alisema wizara inaendelea kuratibu utoaji wa chanjo ya ugonjwa huo kupitia vituo vya kutolea huduma za afya vya umma na binafsi, huduma za mkoba na kampeni.

Alisema vituo 7,200 vya kutolea huduma vinatoa chanjo ya ugonjwa huo nchini na kwamba hadi kufikia Machi, mwaka huu, Watanzania 32,735,546 ambao ni sawa na asilimia 53.4 ya Watanzania wote walikuwa wamekamilisha chanjo dhidi ya ugonjwa huo.

"Chanjo hii imeweza kujenga kinga kwenye jamii, hivyo kupunguza hatari ya kuugua ugonjwa huu na hata waliougua kutopata madhara makubwa," alisema.

Katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu, kumekuwa na wastani wa visa 302 kwa mwezi bila kifo ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka 2021/22 ambapo kulikuwa na wastani wa visa 1,557 na vifo 43 kwa mwezi.

Kadhalika, Waziri Ummy alisema serikali imeendelea kuwalinda wasichana wenye umri wa miaka 14 dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi kwa kununua na kusambaza chanjo ya ugonjwa huo iitwayo Human Papilloma Virusi (HPV) dozi 763,500.

Alisema katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, wasichana 535,708 wenye umri wa miaka 14 ambao ni walengwa wa huduma za chanjo ya kuzuia saratani ya mlango wa kizazi walipatiwa chanjo.

# Tanzania yang'ara matumizi ya TEHAMA

**Na Romana Mallya**

TANZANIA imetajwa kuwa miongoni mwa nchi zinazopiga hatua kubwa katika matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kushika nafasi ya 26 kidunia na ya pili barani Afrika baada ya Mauritius.

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia (WB) kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za serikali na ushirikishwaji wa wananchi (GovTech Maturity Index), unaonyesha namna Tanzania ilivyopanda daraja.

Ripoti hiyo ambayo inatokana na utafiti uliofanyika mwaka 2022 katika nchi 198 duniani, inabainisha kuwa Tanzania imefanikiwa kupanda daraja kutoka kundi B hadi kundi A na kushika nafasi ya 26 ikilinganishwa na mwaka 2021 ambapo ilishika nafasi ya 90.

Kwa upande wa Afrika, utafiti huo ulihusisha nchi 49 ikiwamo Tanzania na matokeo yamebaini kuwa, matumizi ya TEHAMA nchini yamepanda na kufikia asilimia 0.86 wakati Mauritius ina asilimia 0.864.

Utafiti huo unaonyesha Tanzania imepanda kutoka nafasi ya tano mwaka 2021 ambapo ilikuwa nyuma ya Afrika Kusini, Ghana, Kenya and Rwanda hadi nafasi ya pili mwaka 2022.

Katika ukanda wa Afrika Mashariki, kati ya nchi 13 ambazo ni Burundi, Comoros, Djibouti, Somalia, Ethiopia, Sudan Kusini, Sudan, Eritrea, Kenya, Uganda, Rwanda, Seychelles, imekuwa kinara kwa kushika nafasi ya kwanza mwaka 2022 wakati mwaka 2021 ilikuwa ya tatu.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo iliyotolewa mwezi Machi mwaka huu, sekta za elimu, afya, fedha na kilimo ni sekta zinazoongoza katika utoaji wa huduma za serikali kupitia TEHAMA na kurahisisha upatikanaji wa huduma hizo kwa wananchi.

Ripoti hiyo imebainisha kuwa, mafanikio hayo yanatokana na utayari wa serikali wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika taasisi za umma, uwapo wa dira mahususi kuhusu Sera ya TEHAMA, sheria na mikakati madhubuti na utekelezaji unaosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA).

Utafiti huo uliangalia maeneo manne ambayo ni mipango na usimamizi wa TEHAMA serikalini ikiwa ni pamoja na uwapo wa miundombinu ya kuhitafadhia mifumo.

Pia uliangalia miongozo ya kubadilishana taarifa kwa mifumo ya serikali na uwapo wa mifumo shirikishi.

Kadhalika uliangalia ushirikishwaji wa wananchi kupitia majukwaa ya kidijitali kwa kupima utaratibu unaotumika kwa wananchi kutoa maoni kwa njia ya kidijitali, taarifa za wazi pamoja na tovuti za serikali.

Eneo lingine ni uwapo wa nyenzo wezeshi za teknolojia serikalini kwa kuangalia sera ya ubunifu wa teknolojia, sheria na kanuni, ujuzi katika masuala ya dijitali na programu mbalimbali zinazotumika kuimarisha TEHAMA serikalini.

# RC apiga marufuku malori kubeba abiria

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amepiga marufuku matumizi ya magari ya mizigo kubeba abiria kwenye mkoa wake.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya wanafunzi wawili wa Shule ya Sekondari ya Mpalanga, Bahi mkoani hapa kupoteza maisha kwenye ajali ya lori la mizigo lililotumika kubeba abiria.

Katika ajali hiyo, wanafunzi wawili wa kike walifariki dunia hapo hapo. Walipoteza maisha ni Neema Yohana Hoya (17) kidato cha tatu mkazi wa Chidilo na Magreth Juma (19) mkazi wa Nholi.

Mbali na vifo hivyo, wanafunzi 31 walipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwa matibabu na wengine 14 walipatiwa matibabu katika zahanati ya Mpalanga.

Senyamule, alipiga marufuku hiyo juzi alipokuwa akizungumza na wakazi wa wilaya ya Bahi alipotembelea familia za wafiwa kuwapa pole.

Alisema ni wakati wa kuacha kuishi kwa mazoea hasa katika matumizi ya vyombo vya usafiri ili kupunguza athari inapotokea ajali.

Pia alisema serikali ya mkoa wa Dodoma itagharamia matibabu ya majeruhi pamoja na mazishi ya waliofariki dunia kwenye ajali hiyo iliyokatisha ndoto za wanafunzi wawili na kujeruhi wengine 31.

Kadhalika, aliwataka wafiwa kuwa na moyo wa subira katika kipindi hichi kigumu kwao na kuliagiza Jeshi la Polisi kuwachukulia hatua haraka watu wote ambao wamehusika katika ajali hiyo.

"Ndugu zangu nawapa pole kwa niaba ya Mheshimiwa Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan. Tumeguswa sana na misiba hii kwa kupoteza nguvu kazi ya taifa la leo na kesho. Serikali iko pamoja nanyi katika kipindi hiki kigumu na tutaendelea kushirikiana katika wakati huu wa msiba kwa kusimamia mazishi ya marehemu wote," alisema Senyamule.

Mkuu wa Usalama Barabari Wilaya ya Bahi, Mrakibu Msaidizi (ASP) Bakari Ramadhani, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa gari hilo lililobeba wanafunzi hali iliyosababisha gari kumshinda dereva kuacha njia hatimaye kupinduka.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumba moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama wakiangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na Muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-8

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Na vipi Eddy, wao wasimame wakupishe, au waendelee?"

"Acha waendelee. Wao waendelee na upelelezi kama kawaida tu kivyao, na mimi nitafanya kivyangu. Na sitaki hapa nikutane nao, ila waambie tu kuwa Eddy sasa yupo kazini.

Cha umuhimu hapa ni kwamba, idara yenu na yetu zinaingiliana, hivyo kama umeniomba, iandikwe barua rasmi kupelekwa kwa wakubwa wangu. Wao watatoa ruhusa na mimi kuanza kazi, ili lolote likitokea liwe rasmi kimaandishi na kwa manufaa mapana na taifa na wananchi kwa ujumla." Eddy akakumbusha.

"Nashukuru sana Eddy, ukweli sikutegemea kama ungekubali kirahisi hivyo. Hilo ondoa shaka, kabla ya kukupigia juzi nilikaa kikao na wakubwa zangu nikatoa ushauri huo wakaniambia kama atakuwa yupo tayari basi aifanye tu."

"Okay sawa, basi acha niende, nikipata ruhusa rasmi nitaianza mara moja na kuna hatua ambazo zitakuwa nakwambia, lakini kumbuka pia kuna hatua ambazo hazitakiwi kuwekwa wazi, labda mpaka mwisho." Eddy alisema na kusababisha wote wawili kuangua vicheko kwa mara nyingine tena.


Inspekta Frank alibaki na furaha moyoni wimbo mdomoni. Alijua ameutua mzigo kwa mtu anaye ana uwezo wa kubeba mizigo mizito.

Hakuna kesi yoyote au upelelezi wowowe aliowahi kushindwa. Alijua kabisa kuwa kesi sasa imepata mtu. Wakati wao wanaiona ni ngumu, lakini kwa Eddy Kamal, ana aina yake ya upelelezi uliochanganyikana na kipaji cha hali ya juu, baadaye inaonekana ilikuwa ni rahisi. Kifupi ni kwamba alifahamu fika kuwa upele umempata mkunaji.

*******************************

Akiwa ndani ya ofisi yake iliyopo maeneo ya Posta Mpya jijini Dar es Salaam, Eddy aliletewa barua rasmi kwenye idara yake ya kuazimwa kuwasaidia askari polisi uchunguzi wa kifo cha mwanamama Tessy.

Kama kawaida yake hakuanza tu hivi hivi. Alianza na kanuni zinazoongoza mambo ya kipelelezi, kichunguzi na kijasusi.




**Eddy Kamal mpelelezi maarufu nchini, akaendelea kuchambua kabla ya kuanza kazi yake hiyo aina ya tatu ni wadunguaji, 'Snipers.'**

Kwa sababu alisomea mambo ya juu zaidi kuhusu upelelezi, uchunguzi na ujasusi, alijifunza pia aina nane za wauaji na mauaji.

Ili kutaka kung'amua au kuhisi muuaji atakuwa ni nani, ni lazima uende kwenye kanuni hiyo ili anayepata kazi ya kusaka muuaji asianze kukamata kila mtu, hasa wasiohusika.

Kwa unaangalia marehemu ameuawa vipi, mazingira ya kifo na hata eneo ambalo ameuawa. Aina ya kwanza wauaji ni wake wasio na ujuzi. Wao huacha alama kama vile simu, viatu, ndala, leso na kitu chochote ambacho kinaweza kumkamatisha, au wanaopeleleza kuwa na kazi rahisi ya kumng'amua na kumkamata. Huacha alama kwa sababu wao siyo wataalam wa mambo hayo. Labda wamefanya hivyo kwa sababu ya hasira tu. Huwa hawana shabaha kwa sababu wamepewa au kujipa kazi wasioimudu. Hawa wanaitwa kitaalam wanaitwa 'ameurter killers.'

Aina ya pili ya wauaji wao ni wataalam, wanaitwa 'professional killers.' Hawa ni kama wamezaliwa kwa sababu ya kuua. Hawafanyi makosa na hawaoni shida kuua au kutoa uhai wa mtu. Wao kung'oa roho ya mtu ni sawa na kuua mbu.

Eddy Kamal mpelelezi maarufu nchini, akaendelea kuchambua kabla ya kuanza kazi yake hiyo aina ya tatu ni wadunguaji, 'Snipers.'

Haja jamaa ni balaa. Ni wataalam wa kutumia risasi, hawafanyi makosa, hawakopeshi, hawakosea na hupenda kuua wakiwa wamekaa mbali. Hawa wapo kwenye kundi la waliozaliwa kwa ajili ya kuua. Lakini wao wamejikita kwenye eneo moja tu. Kudungua au kuua wakiwa mbali. Anaweza kukaa ghorofani, ukampa kazi ya kumuua mtu. Atakuuliwa unataka apigwe risasi cya kichwa au moyo. Na kweli wanafanya hivyo.

Kundi la nne kuja jamaa wanaitwa 'cold blood killers'. Hawa ni watu wa kuogopwa mno kama ukoma. Ni kama vile hawana roho wala hisia. Ni kama hawakuzaliwa binadamu ila ni wanyama waliojivika ngozi ya binadamu. Wakati mwingine unaweza kusema wana matatizo ya akili. Wao huua taratibu na kwa mateso makubwa mno. Hawa ndiyo wake watu ambao utasikia wamemuua mtu na kuwatenganisha viungo kimoja baada ya kingine. Anaweza kuua kwa leo kukukata kidole, mkono, mguu, kila siku kimoja kimoja hadi mhusika atakapokufa kifo cha mateso. Wapo wanaokwenda mbali zaidi, wanaweza kujirekodi na hata wakati mwingine kupika viungo.

Namba tano ni wauaji kwenye msongo wa mawazo 'stress' au maumivu ya mapenzi. Wauaji hawa hufikia kuona kila mmoja ni adui yake. Anaweza kuchukua silaha na kwenda hadi kwenye kadamnasi ya watu na kuwafyatulia risasi kwa raha zake. Na mara nyingi watu hawa na wao kuishia kujimaliza wao wenyewe watakapobakisha risasi ya mwisho kwenye bastola.

Namba sita inakwenda kwa watu ambao kitaalam wanaitwa 'serial killers.' Hawa ni wahalifu na wavunja sheria wakubwa kwa sababu huanza kwa kuua mtu mmoja tu kwa sababu yoyote ile iwe kulipiza kisasi, wivu wa mapenzi, wizi au chochote kile. Lakini baadaye huendelea kufanya mauaji kwa nyakati tofauti kwa sababu ile ile ama sababu nyinginezo mpaka atakapokamatwa.

Anaweza akaua mtu mmoja tu, lakini akahisi kuna mtu ameuona hivyo ni hatari kwake. Atamsaka mpaka amuue. Mara nyingi wanaua kwa ajili ya kuficha ushahidi ili siri ya kumuua mtu wa kwanza isijulikane. Ataua hata watu zaidi ya 10 kwa sababu ya kuficha siri.

Kundi la saba linaanguka kwa wale wanaoitwa 'licensed to kill'. Wauaji wenye vibali, leseni za kuua.. Hawa huwa ni waajiriwa wa mamlaka za nchi kama yeye mwenyewe Eddy Kamal. Na hufanya hivyo kwa manufaa ya nchi. Wako tayari kufanya chochote kile kwa ajili ya kuilinda na kuitetea nchi ili wananchi waishi kwa amani na utulivu, dhidi ya watu waovu, wasaliti, ambao wapo tayari kuiuza hata nchi au kuhujumu mali za nchi na miundombinu, ikiwemo kutaka kuwafanya wananchi wasiishi kwa amani na utulivu.

Wanyongaji wao wamewekwa kwenye kundi la mwisho wakiitwa 'the hungers.' Tofauti na watu wanavyowafikiria hawa ni watu wema sana, na wanafanya kazi hiyo ikiwa kwao ni ajira rasmi kama zingine. Kazi yao kubwa ni kuwanyonga wahalifu wote waliohukumiwa kunyongwa hadi kufa. Hawa wakati mwingine hufanya ibada pamoja na watu anaotarajia kuwanyonga.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# JKT QUEENS FC YANUSA UBINGWA WA WANAWAKE

Na Adam Fungamwango

JKT Queens imekaribia kutawazwa mabingwa wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Fountain Gate Princess katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma juzi.

Matokeo hayo yanaifanya JKT Queens, mabingwa wa kwanza wa ligi hiyo iliyoanza msimu wa 2016/17 kufikisha pointi 43 na kuiacha Simba Queens ikiwa na pointi zake 42 huku Fountaine Gate Princess iliyoko nafasi ya tatu, ikisalia na pointi zake 38.

JKT Queens inahitaji ushindi dhidi ya timu inayoburuza mkia, Mkwawa Queens yenye pointi tatu bila ya kuangalia matokeo yoyote ya timu nyingine, kila timu imebakiwa na mechi moja mkononi ili kumaliza msimu.

Fountain Gate Princess ndiyo timu pekee iliyokuwa ikitegemewa ingeweza kutoa ushindani au kuizuia JKT Queens kutwaa ubingwa wa ligi hiyo, lakini kipigo ilichokipata kimefifisha kabisa matumaini ya mabingwa watetezi, Simba Queens kutetea taji hilo.

Mbali na matokeo hayo, Alliance Girls ilipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Amani Queens, mechi ikipigwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza huku Yanga Princess ikiwatwanga The Tigers Queens mabao 2-1, kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha wakati Ceasiaa Queens iliibabua Mkwawa Queens magoli 2-0, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Mkwawa, Iringa.

Bingwa wa ligi hiyo atapata nafasi ya kuiwakilisha Tanzania Bara katika mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) ambayo hutoa mwakilishi wa ukanda huo atakayekwenda kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake itakayofanyika baadaye mwaka huu huko Ivory Coast.

Simba Queens pia walikuwa mabingwa watetezi wa CECAFA wakati AS FAR ya Morocco walitwaa ubingwa wa Afrika katika fainali zilizofanyika nchini kwao mwaka jana.




Kiungo mkabaji wa Fountain Gate Princess, Hasnat Ubamba (kushoto), akijipanga kumtoka beki wa JKT Queens, Happyness Mwaipaja katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma juzi. JKT Queens ilishinda mabao 3-0. **PICHA: MTANDAO**

# Ulimboka, Kitumbo jela ya soka

Na Adam Fungamwango

KAMATI ya Maadili ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imewafungia maisha kujishughulisha na masuala ya soka, Mwenyekiti wa Kitayosce FC, Yusuph Kitumbo na kocha, Ulimboka Mwakingwe, baada ya kutiwa hatiani na kosa la upangaji wa matokeo.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya TFF chini ya Ofisa wake, Clifford Ndimbo, jana ilisema wawili hao walijihusisha na upangaji matokeo katika mechi ya Ligi ya Championship kati ya Fountain Gate FC dhidi ya Kitayosce FC iliyochezwa Aprili 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Gairo mkoani, Morogoro.

Kikao cha Kamati ya Maadili kilichofanyika juzi kimewatia hatiani watuhumiwa hao kwa kuzingatia ibara ya 73 (9) (b) ya Kanuni za Maadili za TFF, toleo la 2021.

Kitumbo hakufika mbele ya kamati bila kutoa udhuru wowote wa maandishi ya kupokea wito, wakati Mwakingwe aliwasilisha utetezi wake kwa njia ya maandishi.

Aidha, taarifa imesema uamuzi kamili utatolewa kwa maandishi kwa pande husika katika mashauri hayo mawili.

"Katika barua hiyo ambayo iliambatanishwa na ushahidi wa sauti na picha, Fountaine Gate wanalalamika Aprili 28, mwaka huu, viongozi hao walifanya mbinu chafu za kuwashawishi baadhi ya wachezaji wa Fountain Gate kupanga matokeo kwa kuwatumia fedha." Iliandika sehemu ya taarifa ya klabu hiyo na kunukuliwa na Bodi ya Ligi.

# Polisi Tanzania yaingia msituni

Na Saada Akida

LICHA ya timu yake kuwa katika nafasi ya pili kutoka chini kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara wakiwa na pointi 22, Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Mwinyi Zahera, anapiga hesabu ya kuzichukua pointi tisa ili kujiweka mahali salama.

Zahera alisema anahitaji kushinda katika mechi zote tatu zilizosalia ili kuendelea kubaki katika ligi hiyo na wataanza kwa kuiduwaza Mtibwa Sugar hapo keshokutwa.

Kocha huyo wa zamani wa Yanga alisema bado anaimani na timu yake itafanya vizuri na kuwaondoa wasiwasi mashabiki wao hawatashuka daraja.

"Bado tunaimani ya kufanya vizuri katika hizi mechi tatu zilizosalia kwa kuhakikisha tunavuna pointi tisa zitakazotuondoa hapa chini, tukifanikiwa kupata hizo tutakuwa na alama 31 ambazo ni salama," alisema kocha huyo.

Aliongeza maandalizi ya kikosi chake kuelekea mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar yamekamilika na wataingia kwa tahadhari kwa sababu ndio michezo yao ya fainali iliyobakia.

# Netiboli Arusha yawaza ubingwa

Na Shufaa Lyimo

TIMU ya netiboli ya Polisi Arusha imesema inaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kuhakikisha inafanywa vizuri katika mashindano Ligi Daraja la Kwanza yatakayofanyika kuanzia Juni 2, mwaka huu Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti la Nipashe, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Emerenciana Silas, alisema kikosi chake kilianza maandalizi mapema na amewaandalia mazoezi maalumu wafungaji wake.

"Tumeanza maandalizi yetu mapema kwa sababu ninatambua kutakuwa na ushindani katika ligi hiyo kutokana na wingi wa timu zitakazoshiriki mwaka huu," alisema Silas.

Kocha huyo alisema hana wasiwasi na kikosi chake na hakuna timu yoyote ambayo anaihofia kutokana na kuwaamini wachezaji wake.

"Nina wachezaji wazuri ambao nikiwapa maelekezo yangu wanafanya kama ninavyotaka, tunaomba mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono tutimize malengo yetu, na kwa upande wa uongozi tunatarajia kukamilisha taratibu za kulipa ada ya ushiriki," aliongeza kocha huyo.

**HABARI MICHEZO**

**ZISIKUPITE**

### SPURS KUMBAKISHA KANE

KLABU ya Manchester United inahofia huenda ikakosa kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Harry Kane, msimu huu wa joto, huku Spurs wakidhamiria kumbakisha nahodha huyo wa England mwenye umri wa miaka 29 ingawa hivi karibuni atakuwa amesalia na mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake. (***Mirror***)

### BUSQUETS KUMPISHA MESSI

RAIS wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Javier Tebas, amesema kuondoka kwa kiungo wa kati wa Hispania, Sergio Busquets pale Barcelona ndio "mwanzo wa kuelekea" kwa klabu hiyo kumsajili tena mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 35, ambaye mkataba wake na Paris St-Germain unamalizika katika majira ya joto. (***Cadena COPE***)

### LUKAKU KUREJEA CHELSEA

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, mwenye umri wa miaka 29, atarejea Chelsea kutoka Inter Milan ambako amekuwa kwa mkopo msimu wa joto na kufanya mazungumzo na mkufunzi mpya wa The Blues,Mauricio Pochettino. Pia kushiriki katika mazoezi ya kabla ya msimu kabla ya uamuzi kufikiwa kuhusu mustakabali wake. (***Mirror***)

### POCHETTINO AMTAKA MOUNT

MAURICIO Pochettino anataka Chelsea ianze upya mazungumzo ya mkataba mpya na kiungo, Mason Mount, mwenye umri wa 24, ambaye mkataba wake na The Blues unakamilika mwishoni mwa msimu ujao. (***Standard***)

### UGARTE AGEUKA LULU

KLABU ya Aston Villa ipo katika mazungumzo ya kumsajili kiungo wa kati wa Sporting Lisbon, Manuel Ugarte, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay mwenye umri wa miaka 22 akihusishwa pia na Chelsea na Liverpool. (***Football transfers***)

### PICKFORD KUMRITHI DE GEA

MANCHESTER United Inajiandaa kumnunua mlinda mlango wa Everton na England, Jordan Pickford mwenye umri wa miaka 29, ikiwa kipa wa Hispania, David de Gea (32), ataamua kuondoka katika klabu hiyo. (***Mirror***)

### VERBRUGGEN ATAJWA UNITED

MANCHESTER United inavutiwa na mlinda mlango wa Anderlecht na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Bart Verbruggen, mwenye umri wa miaka 20, baada ya majaliwa ya David De Gea katika klabu hiyo ya Old Trafford kuwa shakani. (***Manchester Evening News***)

### MARTINEZ NJIA MOJA

GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Argentina, Emiliano Martinez, anatarajiwa kuondoka Aston Villa msimu wa joto, huku Chelsea, Manchester United na Tottenham zikimwania mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30. (***Gaston Edul, TyC Sports***)

### INZAGHI, ONANA HAWAONDOKI

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Giuseppe Marotta, anahisi kocha, Simone Inzaghi atasalia katika klabu hiyo na kuongeza kipa wa Cameroon, Andre Onana (27), ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, anataka kusalia katika klabu hiyo ya Serie A. (***La Gazzetta dello Sport***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HENDERSON: LIVERPOOL ITAIMARIKA MSIMU UJAO

**Lakini asema ndoto hiyo itakamilika endapo washambuliaji wao tegemeo...**

**LONDON,** England

NAHODHA Jordan Henderson anaamini Liverpool wanapaswa kuwatumia wafungaji mabao wote waliopo kwa manufaa yao msimu ujao.

**Kurejea katika utimamu wa Luis Diaz katika wiki za hivi karibuni kunamaanisha Kocha, Jurgen Klopp, sasa anaweza kuchagua kati ya washambuliaji watano kati ya sita ambao ni chaguo la kwanza (Roberto Firmino anayeondoka ni majeruhi).**

Hilo limechangia kuimarika kwa kiwango ambacho kimeleta ushindi mara sita mfululizo na kuwafanya waingie katika kuwania nne bora, wakiwa pointi moja nyuma ya Manchester United ambao wamecheza mechi moja zaidi.

Ikiwa wachezaji hao - Mohamed Salah, Darwin Nunez, Diogo Jota, Cody Gakpo na Diaz wanaweza kubaki fiti, Henderson anatarajia Liverpool kuimarika kwa kiwango kikubwa msimu ujao.

"Mambo yanabadilika kila wakati na tumekuwa na wachezaji wapya wanaokuja kwenye safu hiyo ya mbele na ni wachezaji wa kufurahisha sana," alisema akiambia Sky Sports.

"Kuna vitu vingi tofauti tunaweza kutumia na wachezaji tofauti ambao wanaweza kufanya mambo tofauti kweli.

"Tuna wachezaji wengi wenye ubora ambao wanaweza kwenda mbele na wote wanaweza kufunga mabao, hivyo tunahitaji kuwatumia kwa manufaa msimu ujao.

"Limekuwa jambo la kusisimua kwetu msimu huu kuwa waaminifu. Labda tumejitahidi kupata uthabiti kwa walio wengi.

"Jambo zuri ni kwamba tunafanana zaidi na sisi na nadhani bado kuna safari ndefu ya kuboresha kwetu lakini dalili ni nzuri.

"Natumaini tunaweza kumaliza mechi hizi tatu kwa nguvu zaidi."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,112,40

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
DODOMA FC
1 | 1.11
X | 6.21
2 | 16.48

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# UNITED YAMFUKUZIA LAUTARO



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina anayekipiga Inter Milan ya Italia, Lautaro Martinez, ili waweze kumsajili katika dirisha lijalo.

Martinez amekua akionyesha ubora mkubwa ndani ya Inter kwa muda mrefu sasa, huku United wao wakiwa wanatafuta mshambuliaji mwenye ubora mkubwa ili kuboresha safu yao ya ushambuliaji.


United imekua ikitafuta mshambuliaji wa kiwango cha dunia kwa muda mrefu na wanahusishwa na washambuliaji kadhaa kama Harry Kane anayekipiga Tottenham.

Lakini inaelezwa hofu yao kubwa ni huenda wasimpate mshambuliaji huyo wa kimataifa wa England kutokana na ugumu wa bosi wa klabu hiyo, Daniel Levy na sasa wamemgeukia Lautaro.

United iliyoko chini ya kocha Erik Ten Hag inataka kutengeneza timu yenye ushindani mkubwa na kuirudisha kwenye ubora wake.

Mbali na United, Laurato ameshahusishwa na klabu kadhaa kubwa duniani kutokana na aina yake ya uchezaji wake.

# Emery aionya Spurs vita kuwania 4 bora



**LONDON,** England

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, ameiambia Tottenham Hotspur kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya ni ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa hapo awali.

Aston Villa watawakaribisha Spurs leo huku timu hizo mbili zikiwa bado katika harakati za kuwinda kumaliza katika nne bora katika Ligi Kuu England.

Spurs iko katika nafasi ya sita, pointi sita nyuma ya Manchester United walio nafasi ya nne wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Kuchelewa kwa Villa iliyo katika nafasi ya nane ya kuingia katika nafasi ya nne bora kulisababishwa na vipigo vya ugenini vya 1-0 kutoka kwa United na Wolves katika wiki mbili zilizopita.

"Matarajio yao mwanzoni yalikuwa katika nne bora," alisema bosi huyo wa zamani wa Arsenal, Emery.

"Sasa ni ngumu zaidi kuliko ilivyokuwa miaka mitano hadi 10 iliyopita. Sasa kuna timu saba zinazojaribu kumaliza katika nne bora.

"Labda Aston Villa sasa pia. Ni ngumu zaidi."

Kutafuta kwa Tottenham taji la kwanza tangu mafanikio ya Kombe la Ligi mwaka 2008 kumewafanya kumgeukia, Jose Mourinho na Antonio Conte tangu kuondoka kwa Mauricio Pochettino mnamo Novemba, mwaka 2019.

Emery alisema: "Tottenham wamekuwa na matatizo katika mwezi uliopita lakini wana wachezaji wazuri sana.

62,859/-



# SALIM AFURAHIA REKODI YA KUKUMBUKWA SIMBA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kukabidhiwa tuzo ya Mchezaji Bora wa Aprili, kipa namba tatu wa Simba, Ally Salim, amesema ana furaha kubwa kwa sababu ameweka rekodi ya kuwa kipa wa kwanza wa timu hiyo kupata tuzo.

Akizungumza katika hafla ya kukabidhiwa tuzo hiyo, Salim alisema tangu utaratibu wa kutoa tuzo uanze, hakuna kipa yeyote aliyewahi kufanikiwa kutwaa, hivyo ameingia katika vitabu vya kumbukumbu vya klabu ya Simba.

"Nawashukuru sana wadhamini kwa sababu wanapotoa tuzo wanatupa moyo wachezaji kuzidi kupambana," alisema kipa huyo ambaye ametokea kikosi cha vijana chini ya miaka 20 cha timu hiyo.

Salim aliwashinda wachezaji, Kibu Denis na Jean Baleke, ambao ndiyo walikuwa katika kinyang'anyiro cha kuwania tuzo hiyo inayotolewa kila mwezi.

Rekodi zinaonyesha si golikipa namba moja, Aishi Manula wala msaidizi wake, Beno Kakolanya waliowahi kupata tuzo hiyo.

Nyota ya kipa huyo ilianza kuchomoza alipoiongoza Simba katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu iliyomalizika kwa Mnyama kushinda mabao 2-0 na siku sita baadaye, kipa huyo alisimama langoni Simba ikicheza dhidi ya Yanga na kupata ushindi kama huo.

Salim pia alisimama langoni Simba ilipocheza dhidi ya Wydad, nyumbani ikishinda bao 1-0 na ugenini ikaondolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuchapwa penalti 4-3.



Mwanariadha wa upande wa mitupo, Sikujua Mbwembwe, akifanya mazoezi ya kurusha tufe kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete, Dar es Salaam jana kwa ajili ya kujiandaa kuitwa katika kikosi cha Timu ya Taifa ya walemavu. **PICHA: JUMANNE JUMA.**

# *Yanga yajipanga kufunga hesabu*

INATOKA UK 24

ya Ligi Kuu Bara," alisema Nabi.

Naye mshambuliaji nyota wa timu hiyo, Fiston Mayele, alisema haitakuwa mechi rahisi kwa sababu itakuwa na mambo mengi ikiwamo kujihakikishia kutwaa ubingwa.

Mayele alisema watashuka dimbani wakiwaheshimu wapinzani wao na pia watacheza kwa tahadhari kubwa kwa kufuata maelekezo ya benchi la ufundi ili kupata pointi tatu wanazozihitaji.

"Mechi ya kesho (leo) tutaingia kwa nguvu kubwa kuhakikisha tunapata pointi tatu ili kufikia malengo tuliyojiwekea, endapo nikipata nafasi ya kucheza nitahakikisha naipa ushindi timu, sisi sio mashabiki bado tukawa na furaha ya ushindi wa nusu fainali, tumemaliza furaha yetu baada ya mechi na sasa tunahitaji alama tatu dhidi ya Dodoma Jiji FC," alisema Mayele.

Kocha Msaidizi wa Dodoma Jiji FC, Kassim Lyogope, alisema wamejipanga vizuri kwa ajili ya kupambana katika mchezo huo na wanatambua mechi hiyo itakuwa tofauti na mechi waliyocheza katika mzunguko wa kwanza. Lyogope alisema mechi ya leo wataingia kwa utofauti mkubwa kwa sababu timu zote mbili itshuka ikiwa na malengo yake huku akiweka wazi Dodoma Jiji wanahitaji kupata matokeo mazuri ili kujiweka mahali salama katika msimamo.

"Mchezo wa kesho (leo) ni muhimu sana kwa sababu ni wakati muhimu wa kutafuta pointi ili kujinusuru kushuka daraja, tukiteleza katika mchezo huu utaturudisha chini na sisi hatutaki kushuka kwenye nafasi za chini, inatulazimu kupambana kupata matokeo mazuri," alisema Lyogope.

Aliongeza wamefanyia kazi mechi tano za Yanga , hivyo wamejiimarisha kuwazuia kutangaza ubingwa mbele yao.


SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 13/05/23 | 17:00 | Aston Villa vs Tottenham Hotspur | 2.18 | 3.40 | 2.95 |
| 02. 13/05/23 | 17:00 | Southampton FC vs Fulham FC | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 03. 13/05/23 | 17:30 | FC Vizela vs FC Famalicao | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 04. 13/05/23 | 19:15 | Cercle Brugge vs KAA Gent | 2.65 | 3.15 | 2.24 |
| 05. 13/05/23 | 19:30 | Sunderland AFC vs Luton Town | 2.60 | 3.20 | 2.60 |
| 06. 13/05/23 | 19:30 | Villarreal CF vs Athletic Bilbao | 2.17 | 3.35 | 3.00 |
| 07. 13/05/23 | 19:45 | FC Volendam vs Sparta Rotterdam | 2.85 | 3.45 | 2.24 |
| 08. 13/05/23 | 21:30 | CA Independiente Avellaneda vs CA Tigre | 2.44 | 2.90 | 2.60 |
| 09. 14/05/23 | 00:00 | CA Banfield vs CA San Lorenzo de Almagro | 2.47 | 2.80 | 2.65 |
| 10. 14/05/23 | 13:30 | Hellas Verona vs Torino FC | 2.29 | 3.05 | 3.10 |
| 11. 14/05/23 | 14:00 | Coventry City vs Middlesbrough FC | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 12. 14/05/23 | 15:00 | RC Celta de Vigo vs Valencia CF | 2.16 | 3.20 | 3.20 |
| 13. 14/05/23 | 16:30 | VfB Stuttgart vs Bayer Leverkusen | 2.60 | 3.40 | 2.43 |
| 14. 14/05/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs Vitoria SC Guimaraes | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 15. 14/05/23 | 18:05 | AS Monaco vs Lille OSC | 2.60 | 3.50 | 2.37 |
| 16. 14/05/23 | 19:00 | Bologna FC vs AS Roma | 3.15 | 3.00 | 2.28 |
| 17. 14/05/23 | 20:00 | Defensa y Justicia vs Estudiantes de La Plata | 2.26 | 2.85 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 13/05/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1956 | Leeds vs Newcastle | 4.39 | 3.99 | 1.64 |
| 14:30 | 4139 | Rangers vs Celtic | 2.78 | 3.41 | 2.31 |
| 15:00 | 3494 | Real Sociedad vs Girona | 1.61 | 3.76 | 4.91 |
| 16:00 | 1294 | Bloemfontein Celtic vs Moroka Swallows FC | 2.14 | 2.97 | 3.50 |
| 16:00 | 2896 | Salernitana vs Atalanta | 4.49 | 3.89 | 1.64 |
| 16:00 | 3240 | TS Galaxy FC vs Chippa Utd | 2.02 | 3.07 | 3.70 |
| 16:00 | 3678 | Golden Arrows vs Amazulu | 2.30 | 2.98 | 3.13 |
| 16:00 | 4634 | Geita Gold FC vs Mbeya City | 1.80 | 3.11 | 4.09 |
| 16:00 | 5070 | Young Africans vs Dodoma FC | 1.11 | 6.21 | 16.48 |
| 16:30 | 2245 | Zenit St Petersburg vs FC Krasnodar | 1.43 | 4.50 | 5.86 |
| 16:30 | 2521 | Union Berlin vs SC Freiburg | 2.15 | 3.06 | 3.36 |
| 16:30 | 2793 | Bayern Munchen vs Schalke 04 | 1.14 | 7.22 | 13.77 |
| 16:30 | 2915 | VfL Bochum vs Augsburg | 2.08 | 3.49 | 3.09 |
| 16:30 | 4550 | Eintracht Frankfurt vs Mainz | 2.09 | 3.54 | 3.04 |
| 16:30 | 4754 | VfL Wolfsburg vs Hoffenheim | 1.88 | 3.74 | 3.44 |
| 17:00 | 1495 | Manchester Utd vs Wolverhampton | 1.39 | 4.47 | 6.71 |
| 17:00 | 2060 | Aston Villa vs Tottenham | 2.21 | 3.40 | 2.90 |
| 17:00 | 2256 | Chelsea vs Nottingham | 1.47 | 4.20 | 5.80 |
| 17:00 | 2676 | Southampton vs Fulham | 2.70 | 3.25 | 2.43 |
| 17:00 | 2973 | St Mirren vs Hearts | 2.56 | 3.21 | 2.61 |
| 17:00 | 3403 | Aberdeen vs Hibernian | 2.13 | 3.36 | 3.15 |
| 17:00 | 4006 | Crystal Palace vs Bournemouth | 1.83 | 3.50 | 3.89 |
| 17:00 | 4111 | FC Ingulets vs Shakhtar Donetsk | 9.84 | 5.12 | 1.23 |
| 17:00 | 4483 | Kilmarnock vs Livingston | 2.02 | 3.37 | 3.42 |
| 17:00 | 4982 | HJK Helsinki vs Inter Turku | 1.56 | 3.75 | 4.93 |
| 17:00 | 5053 | Seinajoen JK vs Ilves Tampere | 1.79 | 3.33 | 4.00 |
| 17:00 | 5592 | Bolton vs Barnsley | 2.38 | 3.22 | 2.87 |
| 17:00 | 5594 | St Johnstone vs Motherwell | 2.63 | 3.06 | 2.64 |
| 17:15 | 1022 | Osasuna vs Almeria | 2.05 | 3.35 | 3.30 |
| 17:30 | 2850 | FC Vizela vs Famalicao | 2.35 | 3.22 | 2.86 |
| 17:30 | 3998 | GD Chaves vs Pacos Ferreira | 2.09 | 3.32 | 3.27 |
| 18:00 | 2344 | Bodo Glimt vs Rosenborg | 1.35 | 4.81 | 7.33 |
| 18:00 | 2602 | Molde vs Stromsgodset | 1.28 | 5.46 | 8.20 |
| 18:00 | 3440 | Strasbourg vs Nice | 2.33 | 3.24 | 2.84 |
| 18:00 | 3882 | Sandefjord vs Viking | 3.36 | 3.36 | 2.04 |
| 18:00 | 5289 | Sarpsborg vs Brann | 3.47 | 3.47 | 1.97 |
| 18:30 | 4324 | IFK Mariehamn vs Haka | 2.92 | 3.08 | 2.26 |
| 19:00 | 1917 | Spezia vs AC Milan | 3.90 | 3.40 | 1.85 |
| 19:30 | 2565 | Villarreal vs Athletic Bilbao | 2.12 | 3.40 | 3.10 |
| 19:30 | 3531 | Sunderland vs Luton Town | 2.51 | 3.11 | 2.71 |
| 19:30 | 5545 | Borussia Dortmund vs Monchengladbach | 1.22 | 6.37 | 8.56 |
| 19:45 | 1570 | FC Volendam vs Sparta Rotterdam | 2.90 | 3.45 | 2.20 |
| 20:00 | 3722 | Portimonense vs Benfica | 10.07 | 5.84 | 1.23 |
| 21:45 | 2794 | Inter vs Sassuolo | 1.39 | 4.69 | 6.39 |
| 22:00 | 2271 | Paris St Germain vs AC Ajaccio | 1.13 | 6.82 | 17.06 |
| 22:00 | 4021 | Bahia BA vs Flamengo | 3.07 | 3.36 | 2.10 |
| 22:00 | 4194 | Utrecht vs Waalwick | 1.55 | 4.30 | 4.70 |
| 22:00 | 5597 | Real Madrid vs Getafe | 1.58 | 3.74 | 5.31 |
| 22:00 | 5939 | Wydad Casablanca vs Mamelodi Sundowns | 2.05 | 3.25 | 3.10 |
| 22:30 | 2367 | Sporting Lisbon vs Maritimo | 1.19 | 6.20 | 12.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Mei 13, 2023




UK. 22

United yamfukuzia Lautaro



Mshambuliaji wa Azam FC, Prince Dube (kulia), akijipanga kumtoka mchezaji mwenzake wa timu hiyo katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Namungo itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# YANGA YAJIPANGA KUFUNGA HESABU

**Na Saada Akida**

## ●●● Nabi ataka kutangaza ubingwa leo huku Dodoma Jiji ikikataa...

KIKOSI cha Yanga kinatarajia kuikaribisha Dodoma Jiji FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam ikiwa imejipanga kukamilisha mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo kwa msimu huu wa 2022/2023.

**Endapo Yanga yenye pointi 71 ikipata ushindi leo, tayari itaku wa imefanikiwa kutetea taji hilo wanalolishikilia huku wakiwa na mechi mbili mkononi kwa sababu itafikisha pointi 74 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote.**

Watani zao ambao walikuwa wakiwapa presha katika mbio hizo, Simba yenye pointi 64, watafikisha pointi 73 tu endapo watashinda mechi zao tatu zilizobakia.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia Nipashe anaupa umuhimu mkubwa mchezo huo ingawa anatarajia kufanya mabadiliko kidogo katika kikosi chake na hii inatokana na kutaka kuwapa nafasi nyota ambao hawakucheza mara kwa mara.

Nabi alisema wanatarajia kupambana na kucheza kwa juhudi katika mechi ya leo kwa sababu inatoa tafsiri ya kutwaa ubingwa hivyo wachezaji wake wanafahamu wanatakiwa kupambana ili kupata matokeo mazuri.

"Kuna wachezaji wamechoka na wana majeraha, nitawapa nafasi wale ambao hawajacheza mara kwa mara, kikubwa nawaomba wachezaji kujituma kwenye mchezo wa kesho (leo), mechi ya mzunguko wa kwanza wachezaji hawakuwa na mechi ya kimataifa.

Nawaomba wachezaji kutowadharau Dodoma Jiji FC kwa sababu wamefanikiwa kushinda mchezo wa hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika," alisema Nabi.

Kocha huyo aliongeza mechi ya leo itamsaidia kiufundi kuelekea mchezo wa nusu fainali ya pili na kama wakishinda itawaongezea nguvu kwa sababu watakuwa wameshatangazwa mabingwa wapya.

"Tunahitaji ushindi ili tunapokwenda Afrika Kusini hatutakuwa na presha juu ya matokeo ya michezo miwili iliyosalia

INAENDELEA UK 23

# Simba: Baleke ni wetu

**Na Saada Akida**

WAKATI kukiwa na tetesi za mshambuliaji wa Simba, Jean Beleke, kutakiwa na klabu ya Ulaya, mabosi wa Wekundu wa Msimbazi wamesema nyota huyo ni mali yao na timu yoyote inayomhitaji, itatakiwa kufuata taratibu.

Simba ilimsajili Baleke kwa mkataba wa mkopo wa miaka miwili akitokea TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), na kwa kipindi kifupi ameisaidia timu hiyo katika mashindano mbalimbali.

Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana Beleke ana mkataba na klabu yao na kwa sasa wao ndio wanaotakiwa kutoa baraka kwa timu nyingine itakayojitokeza kuhitaji huduma ya Mkongomani huyo.

Ahmes alisema endapo TP Mazembe wamepokea ofa ya kumhitaji mshambuliaji huyo, mabingwa hao wa zamani watalazimika kufanya mazungumzo na Simba kuhusu mchakato huo na hatimaye kufikia makubaliano.

"Ni kweli Baleke yuko Simba kwa makubaliano maalum ambayo tumefanya na TP Mazembe, lakini endapo kuna ofa imewafikia wanatakiwa kutuambia na kama watamuuza bila kutujulisha watalazimika kurejesha fedha zetu kulingana na makubaliano tuliyoingia," alisema Ahmed.

Aliongeza Simba inatakiwa kushirikishwa juu ya mauzo ya nyota huyo ila kwa sasa wanatambua bado ni mchezaji wao halali kutokana na mkataba ambao walikubaliana na TP Mazembe.

"Kuhusu TP Mazembe kupokea barua ya ofa hatuna taarifa nayo, kwa sasa siwezi kuweka wazi kwa sababu taarifa hizo bado hazijafikia mezani kwangu, tutaweka wazi taarifa juu ya ofa hiyo ya Baleke kuondoka Simba muda utakapofikia," Ahmed alisema.

Baleke aliyejiunga Simba katika dirisha dogo amefunga mabao nane wakati kinara ni Fiston Mayele wa Yanga ambaye amezifumania vyavu za wapinzani mara 16.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >